BREAKING NEWS
SUPA JACKPOT
1,023,154,178
KWA 1000/- TU!
SportPesa.CO.TZ | PIGA *150*87#



**Ridhiwani** aingia mitaani kutatua migogoro ardhi

UKURASA 3

TANZANIA SENSA 23 Agosti 2022 Jiandae Kuhesabiwa


# Nipashe

Jumamosi Agosti 20, 2022 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0581043

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US




## Neville amsihi Ronaldo

UKURASA 22

# Wastaafu NSSF kulipwa bil. 829/-



UKURASA 2



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa (wa pili kushoto), akiziaga kaya 25 zenye watu 105 zinazohama kwa hiari kutoka Ngorongoro katika ofisi za Mamlaka ya Hifadhi ya Eneo la Ngorongoro, Karatu mkoani Arusha jana, kwenda Kijiji cha Msomera, Handeni mkoani Tanga. Kushoto ni Mkuu wa Mkoa wa Arusha, John Mongela. **PICHA: OWM**

## YALIYOMO

UKURASA WA 2

### KORTINI MADAI WIZI MABILIONI YA BENKI

WAFANYABIASHARA wawili wamepandishwa kizimbani katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu wakikabiliwa na mashtaka manne likiwamo la kuingilia mfumo wa Benki ya BancABC ...

UKURASA WA 4

### KITUO UCHUNGUZI SARATANI KUJENGWA

KITUO cha kisasa cha kutoa huduma za uchunguzi wa ugonjwa wa saratani kinatarajia kujengwa nchini ambacho kitakuwa na uwezo wa kugundua...

## Waziri aagizwa kumwondoa kigogo madai ya kukwamisha maendeleo

UK. 2

## TRC yaomba ongezeko la nauli za treni

UK. 3

MICHEZO MNIGERIA KUTUA SIMBA UK.24 MAONI, KATUNI UK.6



Mkurugenzi wa Kodi wa KPMG Tanzania, Nsanyiwa Donald, akitoa mada kwenye mkutano wa sekta binafsi wa mwaka 2022, ulioandaliwa na Baraza la Biashara la Afrika Mashariki (EABC), jijini Dar es Salaam jana, baada ya bajeti na uhuishaji kwenye masuala ya ushuru wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC). **PICHA: MIRAJI MSALA**

# NSSF kulipa bil. 829/- wastaafu

**Na Fatuma Athumani, TURDACO**

MFUKO wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF) katika mwaka wa fedha 2022/23, unatarajia kulipa mafao ya Sh. bilioni 828.91 kwa wanachama wastaafu na wanufaika wengine 101,846.

Malipo hayo ya mafao ni ongezeko la asilimia 26 kulinganisha na Sh. bilioni 659.76 zilizolipwa katika mwaka wa fedha ulioishia Juni 2022.

Mkurugenzi Mkuu wa NSSF, Masha Mshomba, aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu utendaji wa mfuko kwa mwaka wa fedha wa 2022/23.

Alisema pia mfuko utaendelea kuimarisha mifumo na usimamizi wa fedha ili kuepuka mianya ya upotevu na kuuwezesha kumudu gharama za uendeshaji na kulipa mafao.

Mshomba alisema lengo kuu la usimamizi wa fedha ni kutunisha mfuko kwa ajili ya kuwa na uwezo wa kulipa mafao kwa wanachama wake kwa mujibu wa sheria.

Sambamba na hilo, alisema wataongeza mapato yatokanayo na uwekezaji na kukamilisha miradi ya uwekezaji

Katika kuhakikisha thamani ya michango ya wanachama inalindwa, alisema mfuko huwekeza katika maeneo mbalimbali ikiwamo hatifungani, hisa, mikopo, miundombinu, miliki ardhi na amana za benki.

Alisema katika mwaka huo, mfuko unatarajia kukusanya Sh. bilioni 691.04 kutokana na mapato ya uwekezaji na ongezeko la thamani ya vitega uchumi.

Mshomba alisema pia mfuko umeweka kipaumbele kwa uwekezaji wa maeneo salama na yenye faida zaidi ili kulinda fedha za wanachama wa mfuko.

Mbali na mkakati huo, alisema mfuko unatarajia kukamilisha miradi yake ya majengo biashara yaliyoko Dar es Salaam na Mwanza na nyumba zilizoko Kigamboni.

Alisema mradi wa jengo la biashara kwa matumizi ya hoteli ya kitalii ulioko jijini Mwanza, umefikia asilimia 74 na ujenzi wake unatarajiwa kukamilika ifikapo Juni, mwakani.

Mshomba pia alisema mradi wa jengo la biashara kwa matumizi ya makazi na hoteli (Mzizima Tower) ulioko jijini Dar es Salaam, umefikia asilimia 90 kwa jengo la makazi na asilimia 84 kwa jengo la hoteli. Alisema ujenzi wa mradi huo unatarajiwa kukamilika ndani ya mwaka wa fedha 2022/23.

Kuhusu miradi ya nyumba za makazi Mtoni Kijichi, Dungu na Toangoma mkoani Dar es Salaam, alisema imefikia asilimia 77 ya ujenzi na inatarajiwa kukamilika ifikapo Juni, 2023.

Kadhalika alisema kwa mwaka huo wa fedha, thamani ya vitega uchumi vya mfuko (Investment portfolio) inatarajiwa kukua na kufikia Sh. trilioni 6.1 ikiwa ni ongezeko la asilimia 17 ukilinganisha na thamani ya Sh. trilioni 5.2 iliyofikiwa katika mwaka wa fedha ulioishia Juni, 2022.

# Kortini madai wizi mabilioni ya benki

**Na Grace Gurisha**

WAFANYABIASHARA wawili wamepandishwa kizimbani katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu wakikabiliwa na mashtaka manne likiwamo la kuingilia mfumo wa Benki ya BancABC na kuiba zaidi ya Sh. bilioni 1.6.

Akisoma hati ya mashtaka, Wakili wa Serikali Gloria Matemu, alidai jana mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu Richard Kabate kuwa washtakiwa wanadaiwa kutenda makosa hayo kati ya Oktoba Mosi, mwaka jana na Julai 31, mwaka huu.

Matemu alidai kuwa katika shtaka la kwanza, washtakiwa wanadaiwa kati ya Oktoba Mosi, 2021 na Julai 31, walikula njama nje ya Tanzania kutenda kosa la wizi.

Katika shtaka la pili, alidai washtakiwa hao isivyo halali na kwa makusudi, waliingilia mfumo wa benki wa kompyuta na kuutumia.

Alidai katika shtaka la tatu, katika miji ya Arusha na Dar es Salaam na ndani ya Tanzania, Uganda, Ghana na Ivory Coast, waliiba fedha hizo kutoka kwenye kitambulisho cha benki hiyo mali ya BancABC.

Katika shtaka la nne, inadaiwa washtakiwa hao walijipatia Sh. 1,600,000,000 mali ya African Banking Corporation Tanzania Ltd (BancABC) huku wakijua zimetokana na zao la wizi.

Baada ya washtakiwa kusomewa mashtaka hayo, hawakutakiwa kujibu chochote kwa sababu Mahakama ya Kisutu haina mamlaka ya kusikiliza kesi hiyo ya uhujumu uchumi.

Wakili wa Serikali Mwandamizi, Grace Mwanga, alidai kwamba upelelezi wa kesi hiyo bado unaendelea, hivyo wanaomba tarehe nyingine ya kutajwa.

Kesi hiyo iliahirishwa hadi Septemba Mosi, mwaka huu kwa ajili ya kutajwa na washtakiwa wamerudishwa mahabusu.

# Waziri aagizwa kumwondoa kigogo kwa madai kukwamisha maendeleo

**Na Beatrice Shayo,** TABORA

CHAMA Cha Mapinduzi (CCM) kimemwagiza Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe, kumwondoa Mrajis wa Vyama vya Ushirika mkoani Tabora, Abou Cheliga, kwa madai ya kuwa kikwazo kwa maendeleo ya ushirika kutokana na kutengeneza urasimu, hivyo kukwamisha jitihada za Rais Samia Suluhu Hassan.

Katibu wa Halmashauri Kuu ya Taifa (NEC) ya CCM, Itikadi na Uenezi, Shaka Hamdu Shaka, alitoa agizo hilo jana akiwa Wilaya ya Uyui, akizungumza na wananchi ambao walimlalamikia mrajis huyo kwamba anawakwamisha kimaendeleo.

Shaka alisema haiwezekani kila wilaya aliyotembelea wanamlalamikia mrajisi huyo kuwa ni kikwazo kwao.

"Hili limekuwa donda sugu. Tumetoka Kaliua analalamikiwa huyu mrajisi, tumetoka Sikonge analalamikiwa huyu bwana, Urambo analalamikiwa na leo (jana) tupo Uyui watu wanalia na huyu mrajis," alisema Shaka.

Alisema urasimu umekuwa mkubwa, utitiri na ukiritimba umekuwa tatizo hali inayosababisha kudumaza jitihada za maendeleo.

"Huko tunakotoka hajasajili vyama kwa sababu kuna mawakala wanapita chini kwa chini. Mbunge amesema na mimi taarifa ninazo wako mawakala wanawahamasisha wananchi wakajiunge chama fulani yeye ndiyo kazi yake. Hilo si jukumu lake la nani akajiunge ushirika gani," alisema.

Shaka alisema kuna vyama vya ushirika 18 havijasajiliwa na kwamba amesajili saba kwa sababu ya mawakala aliowaweka, hali inayoonyesha kunatengenezwa njia za rushwa ambazo serikali inapiga vita.

"Maelekezo yetu kwa Waziri wa Kilimo amwondoe mara moja huyo mrajis wa vyama vya ushirika. Tabora inaongoza kwa kilimo cha tumbaku, hatuwezi kuona jitihada za Rais zinakwamishwa na mtu mmoja halafu tukaendelea kuchekeana, hili halipo," alisisitiza Shaka. "Waziri wa Kilimo tutamjulisha leo (jana) huyu mtu hafai kuwa Tabora wampangie majukumu mengine sehemu ambayo hakilimwi kilimo cha tumbaku. Tuko tayari kulinda jasho lenu na jitihada za Rais Samia anazoziweka ili kukuza zao hili la tumbaku," alisema.

Shaka alisema Rais Samia ameongeza ushindani katika zao hilo kutoka kampuni mbili hadi sita, lakini anatokea mjanja anataka kukwamisha jitihada hizo. Pia alisema kuna haja ya kuangalia uwezekano wa kujenga kiwanda kwa ajili ya kuchakata tumbaku mkoani Tabora pamoja na cha kutengeneza sigara.

Shaka alisema kuna mikoa 12 inayolima tumbaku nchini na mwaka wa fedha 2019/20 zilizalishwa kilo milioni 37 za tumbaku na mwaka wa fedha 2021/22 kilo milioni 140. Alisema mkoa wa Tabora umeongoza katika kilimo cha tumbaku kutoka kilo milioni 16 hadi kufikia kilo milioni 33.

Aidha, Shaka alisema katika mkoa wa Tabora kuna changamoto ambayo amejulishwa kuhusu bei ya mbolea ya ruzuku ambayo inauzwa Dola 70 za Kimarekani.

"Hii bei si sahihi, Rais Samia amewapunguzia makali kutoka Sh. 170,000 hadi kufikia Sh. 70,000 haya yote yanakwenda ndivyo sivyo kwa sababu hakuna usimamizi mzuri unaoeleweka," alisema.

Shaka aliwaagiza viongozi wote wanaohusika waende kusimamia bei elekezi ya serikali, Rais Samia ameamua kuwapunguzia ukali wa maisha wakulima wa tumbaku amepunguza ruzuku kwenye tumbaku.

Alisema lengo la kufanya hivyo ni kuongeza uzalishaji na pato la mwananchi kukua na pato la taifa liongezeke kupitia kilimo hicho cha tumbaku.

Alisema kwenye kuuza mbolea za ruzuku lazima kuwapo na usimamizi nzuri wajanja wote wadhibitiwe ambao wanataka kuhujumu jitihada za Rais Samia katika kuwapunguzia ukali wa maisha wakulima wa tumbaku.

**AJITETEA**

Cheliga alipohojiwa kwa njia ya simu, alisema hakuna ukweli kuhusiana na tuhuma hizo na kinachotokea kwa sasa ni msukumo wa kisiasa.

Alisema anasajili vyama kwa kuzingatia vigezo na sheria na amekuwa akisimamia kwa weledi lakini watu wanatumia fursa kumchafua.

"Nasajili vyama kwa kuzingatia vigezo na sheria na nimekuwa nikisimamia weledi, ninachojua kama unafanya kazi zinazogusa watu malalamiko hayakosekani... na kinachoendelea sasa ni upepo wa kisiasa watu wanatumia fursa kunichafua," alisema.




Mtendaji Mkuu wa Tanzania Mortgage Refinance Company Ltd, Oscar Mgaya (kushoto), akibadilishana mikataba na Makamu wa Rais wa Afrika Habitat for Humanity International, Maurice Makoloo (kulia), jijini Dar es Salaam juzi, baada ya kutiliana saini makubaliano ya kutafuta ufumbuzi wa tatizo la nyumba kwa watu wa kipato cha chini. Katikati ni Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Ridhiwani Kikwete. **PICHA: ROMANA MALLYA**

# Ridhiwani aingia mitaani kutatua migogoro ardhi

**Na Idda Mushi,** MOROGORO

NAIBU Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Ridhiwani Kikwete, ameingia mitaani kwa kuzifuata familia zenye migogoro ya ardhi ya muda mrefu kwa nia ya kujionea uhalisia wa matatizo yao na kupata maelezo ya kina kabla ya kizitafutia ufumbuzi.

Ridhiwani alifanya hivyo juzi mjini hapa kwa kutembelea baadhi ya maeneo yenye migogoro ya ardhi zikiwamo familia za Felician Bupilipili na Rajabu Kyara ambao wamekuwa wakigombea kiwanja Na. 1 na Na. 3 3 vilivyoko mtaa wa Boma Road Manispaa ya Morogoro.

Naibu Waziri huyo alifika katika nyumba hiyo na kumkuta Neli Lukwaja ambaye ni mke wa Bupilipili na kumtembeza maeneo yote ya nyumba ambayo wamekuwa wakiimiliki kwa muda mrefu huku akilalamika kutotendewa haki na Kyara ambaye naye anadai kumilikishwa kwa hati.

Baada ya kutembelea makazi hayo, alielekeza kuitwa kwa familia zote mbili ili kuwasikiliza kwa kina na kutafutia ufumbuzi mgogoro wao katika kikao chake alichokifanya katika Chuo cha Ardhi cha Morogoro (ARIMO).

Katika kikao hicho, Naibu Waziri aliwashirikisha maafisa kutoka Ofisi ya Kamishna wa Ardhi Msaidizi Morogoro na maofisa wa sekta ya ardhi kutoka Manispaa ya Morogoro ili kupata maelezo ya kina ya chanzo na sababu za mgogoro huo.

Baada ya kusikiliza kwa kina, alimwagiza Mkurugenzi wa Upimaji na Ramani wa Wizara, Hamduni Mansour kuja kupitia upya ramani na mipaka ya viwanja hivyo vyenye mgogoro.

# TRC yaomba ongezeko nauli za treni

**Na Maulid Mmbaga**

BARAZA la Ushauri la Watumiaji wa Huduma za Usafiri Ardhini (LATRA-CCC), limesema limepokea maombi ya ongezeko la nauli za treni kwa asilimia 15 kwa kila daraja kutoka Shirika la Reli Tanzania (TRC), kutokana na kupanda kwa bei za mafuta.

Hata hivyo, LATRA-CCC imesema haioni kama kuna haja ya ongezeko hilo huku Chama cha Kutetea Abiria (CHAKUA) kikitaka shirika hilo lijikite kuboresha huduma zake.

Katibu Mtendaji wa LATRA-CCC, Leo Ngowi, akizungumza jana jijini Dar es Salaam wakati wa mkutano wa wadau kujadili nauli za treni ya abiria ya reli ya kati kwa lengo la kukidhi huduma za uendeshaji za TRC, alisema baada ya kupokea maombi hayo, walifanya utafiti mikoa mbalimbali.

Ngowi alisema wamefanya utafiti katika mikoa ya Dar es Salaam, Mwanza, Kigoma na Arusha na kubaini kuwa licha ya TRC kuhitaji ongezeko hilo la nauli, huduma zake hazikidhi mahitaji ya abiria kutokana na mabehewa mengi kupata ajali.

Pia alisema walibaini abiria wao hawapati fursa ya kukata tiketi kwa njia ya mtandao mpaka waende kwenye ofisi zao jambo ambalo limelalamikiwa kuongeza gharama kwa wasafiri.

“Wakati mwingine uhitaji wa tiketi huwa mkubwa lakini abiria hawazipati kwa sababu wahusika hawana uwezo wa kusafirisha abiria,” alisema.

Ngowi alisema malalamiko mengine usafiri wa treni kutopatikana kwa wakati pindi unapohitajika na kusababisha abiria kukaa vituoni muda mrefu na kuongezewa gharama.

“Kutokana na upungufu huu, wananchi wamependekeza badala ya TRC kupeleka maombi ya kuongeza nauli, kwanza waboreshe huduma zao,” alisema.

Akiwasilisha msimamo wa baraza hilo, Ngowi alisema ni kweli gharama za mafuta zimepanda lakini hakuna haja ya TRC kuomba ongezeko la bei badala yake waongeze uzalishaji, waruhusu abiria kukata tiketi kwa njia ya mtandao ili kuwapunguzia wateja gharama na muda wa kusubiri vituoni.

Ngowi alisema baada ya TRC kutekeleza hayo, wanaweza kuwasilisha ombi la kuongeza nauli.

Mwakilishi wa Kaimu Mkurugenzi wa Maendeleo ya Biashara TRC, Hassan Shaaban, alisema wamependekeza kiasi cha asilimia 15 kwa kuzingatia hali ya maisha ya Watanzania wanaotegemea usafiri huo.

“Kuanzia Machi hadi Agosti, ongezeko la bei za mafuta limefika zaidi ya asilimia 38. Tumependekeza ongezeko la asilimia 15 kwa kuangalia hali ya Watanzania wanaotegemea usafiri huu wa reli,” alisema.

Mwenyekiti wa CHAKUA, Hassan Mchanjama, alisema hawakutarajia TRC iombe kuongezewa nauli kwa hali wanayojionea kwenye usafiri huo wa treni.

Alisema kiasi cha abiria wanaobebwa kinazidi asilimia 200 na wamekuwa wakijazana kwenye behewa kupita kiasi.

“Kuna watu wengi wanazamia kwenye treni njiani, tulishawahi kutoa ushauri kwa TRC kwamba kuna haja ya kushirikiana kudhibiti mapato ndani ya usafiri huu kwa sababu unategemewa na watu wengi, behewa moja la daraja la chini wanachukua abiria zaidi ya 800, idadi ambayo ni nusu ya namba halali inayotakiwa iwepo,” alisema.

Mchanjama aliitaka TRC kujipanga zaidi kudhibiti mapato ili waweze kujiendesha vizuri badala ya kutaka nyongeza ya nauli.

german cooperation
DEUTSCHE ZUSAMMENARBEIT

Implemented by: giz Deutsche Gesellschaft für Internationale Zusammenarbeit (GIZ) GmbH

**Support to a capacity needs assessment on pandemic preparedness and response with a One Health approach in the East African Community (EAC)**
**Tender BID No. GIZ/GPPOH/2022/83417295**

**TENDER INVITATION**
**FOR**
**CAPACITY NEEDS ASSESSMENT AMONG A MULTI-SECTORAL AND MULTI-DISCIPLINARY PANDEMIC PREPAREDNESS AND RESPONSE WORKFORCE IN THE EAC REGION.**

On behalf of the Federal Ministry of Economic Cooperation and Development (BMZ), the GIZ Global Programme for “Pandemic Prevention and Response, One Health” (GP PPOH) aims to strengthen national, regional and global capacities for epidemic prevention and response with the One Health (OH) approach. It is based on the BMZ’s One Health Strategy, which identified interfaces between biodiversity, environmental, human and animal health for pandemic prevention and places a special focus on the detection and control of novel zoonoses.

Within the framework of the Global Programme, there is a regional package which aims to support the institutionalisation of the OH approach in the East African Community (EAC). It also aims at strengthening and expanding capacities at the individual, organizational and societal level in the field of pandemic preparedness and response with a OH approach based on regional needs and priorities

In close cooperation with the EAC structures and partners, the GP PPOH seeks to engage a regional consultant to conduct a capacity needs assessment in order to identify specific capacity needs among relevant multi-sectoral and multi-disciplinary pandemic preparedness and response workforce at different levels in the EAC region and EAC Partner States. This will serve as a basis for the GP PPOH to inform the development and/or scale up of relevant capacity development interventions and subsequently, targeted advisory services.

GIZ invites regional consultants with the required knowledge, skills and experience in the area of capacity development, particularly in higher education, continuous professional development, designing capacity development tools and conducting capacity needs assessments. The regional consultant should be equipped with general professional knowledge in the area of pandemic preparedness and response, One Health (PPOH). Experience in the EAC region as well as cooperation experience with development partners and projects in PPOH is key.

**Interested candidates should request for detailed tender documents from giz-tanzania@giz.de no later than 26th August 2022 and submit Technical and Financial proposals by email no later than 5th September 2022.**

217/002002

# Waziri afagilia mpango wa utetezi wanawake

**Na Romana Mallya**

SERIKALI imesema mpango wa Shirika la Umoja wa Mataifa la Masuala ya Wanawake (UN Women) wa utetezi wa haki za wanawake kuhusu uendelevu wa haki ya kijamii Tanzania, utasaidia kuweka mikakati ya kushughulikia kero za UVIKO-19 na kudhibiti majanga mengine yanayoendelea kwa maslahi ya wanawake na wasichana.

Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Dk. Dorothy Gwajima, aliyasema hayo juzi jijini Dar es Salaam wakati akiuzindua mpango huo.

Alisema mpango huo unatoa fursa kujadili hitaji la kuongezeka kwa upatikanaji wa kazi zenye staha kwa wanawake, hifadhi ya jamii na usalama wa chakula na kuongeza kuwa pia unatoa fursa kujadili maeneo matatu muhimu kwa kuzingatia ahadi za Tanzania katika kutekeleza usawa wa kijinsia.

Waziri alisema unasaidia uwekezaji wa umma katika uchumi wa matunzo, kuhakikisha huduma bora za utunzaji ambazo ni muhimu kusaidia wanawake katika nguvu kazi.

Kadhalika, alisema unatoa hatua za haraka na imara za kuwezesha kuwa na uchumi wa buluu na kutumia mageuzi ili kukuza usawa wa kijinsia.

Pamoja na mambo mengine, alisema mpango unatoa namna bora ya kushughulikia changamoto za kijinsia nyakati hizi na ni nyenzo muhimu itakayosaidia kutafakari kinachofanyika na kuweka mikakati ya kusonga mbele.

"Hii ni kwa sababu wanawake na wasichana wanapata athari kubwa kutokana na majanga haya, hivyo tunahitaji kutambua na kushughulikia mahitaji yao ipasavyo," alisema.

Waziri Gwajima aliipongeza UN Women kwa kuendelea kuunga mkono jitihada za serikali katika kukuza usawa wa kijinsia na uwezeshaji wa wanawake.

Alisema janga la UVIKO -19 lilidhoofisha utoaji wa huduma za umma na kusababisha ugumu wa maisha hasa katika eneo la uchumi.

"Shughuli na kazi zisizo za malipo ambazo hufanywa na wanawake na wasichana kwenye familia na jamii zimekuwa ndiyo tegemeo. "Ingawa Tanzania haikukabiliwa na athari mbaya kwa kiwango sawa na dunia nzima, ambako kulikuwa na changamoto za uchumi, matatizo ya huduma za matunzo na kuongezeka kwa viwango vya ukatili wa kijinsia, miongoni mwa mengine, wanawake waliathirika zaidi UVIKO-19," alisema.

Pia alisema Tanzania inakabiliwa na athari ya janga la hali ya hewa na mabadiliko ya tabia nchi na kusababisha changamoto ya majisafi, kilimo, miundombinu na afya.

Waziri huyo alisema kuna sababu kubwa kuwa na sera, mipango na mikakati ambayo moja kwa moja inakwenda kujibu mahitaji ya wanawake na wasichana.

Alisema uzinduzi huo unalenga kuunda jukwaa la majadiliano kwa nia ya kuleta mitazamo chanya ya kuhakikisha kuna kuwa na sera, mipango na mikakati, inayozingatia jinsia ili kuwapatia maisha endelevu na ustahimilivu kwa wanawake dhidi ya majanga yanayoweza kujitokeza.

Mwakilishi Mkazi wa UN Women Tanzania, Hodan Addou, alisema uzinduzi huo wa kitaifa umeandaliwa kwa kuzingatia mwaka mmoja wa utekelezaji wa Jukwaa la Mpango wa Usawa wa Kizazi Tanzania katika kuendeleza haki za kiuchumi za wanawake, kwa lengo la kutoa jukwaa la majadiliano kuhusu mafanikio ya nchi katika haki za kiuchumi.

Pia alisema kutafakari changamoto za sasa za kiuchumi na kuleta mitazamo ya ngazi ya nchi ili kuhamasisha sera na mikakati inayozingatia jinsia, urejeshaji endelevu na kuimarisha ustahimilivu wa wanawake dhidi ya majanga mengine.

Addou alisema UVIKO-19 umeangazia migogoro inayoingiliana ambayo inadhoofisha usawa wa kijinsia na kutishia maisha ya watu.

Hafla hiyo ilishirikisha wawakilishi 60 kutoka sekta binafsi, washirika wa maendeleo na asasi za kiraia ambao walitoa wito wa kuchukuliwa hatua za haraka kushughulikia ajira, uchumi wa matunzo na hali ya hewa kwa manufaa ya wanawake na wasichana.




Mkuu wa Wilaya ya Iringa, Mohamed Moyo (wa pili kulia), akikata utepe kuzindua duka jipya la Tigo, wilayani humo jana. Kulia ni Mkurugenzi wa Tigo Nyanda za Juu Kusini, Abbas Abdulrahman. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Kituo uchunguzi saratani kujengwa Tanzania

**Na Romana Mallya**

KITUO cha kisasa cha kutoa huduma za uchunguzi wa ugonjwa wa saratani kinatarajia kujengwa nchini ambacho kitakuwa na uwezo wa kugundua tatizo hilo katika hatua za awali na kutibu.

Mkataba wa ujenzi wa kituo hicho ulitiwa saini jana katika ubalozi wa India nchini ukihusisha Hospitali ya Apollo ya India na Kampuni ya Eclipse Group Africa ya Dar es Salaam.

Wengine walioshuhudia tukio hilo la utiwaji saini ni Balozi wa India nchini Tanzania, Binaya Pradhan na Naibu Katibu Mkuu, Wizara ya Afya na Ustawi wa Familia ya India, Lav Agarwal.

Akizungumza baada ya kutiwa saini makubaliano hayo, Mwenyekiti wa Eclipse Group Africa, Zahir Damji, alisema hadi sasa tayari wameshapata kiwanja eneo la Msasani kwa ajili ya ujenzi wa kituo hicho.

Alisema kituo hicho kitapoanza kutoa huduma, kitahudumia nchi zote za Afrika na kupunguza gharama za wagonjwa kusafirishwa India kwa ajili ya huduma za saratani kwa kuwa watakuwa wanazipata Tanzania.

"Wagonjwa 2,500 wa saratani kutoka Tanzania wanasafiri kwenda India kila mwaka kutafuta matibabu ambayo yameifanya India kuwa utalii wa kitabibu. Tumeamua kujenga kituo cha saratani hapa kitakuwa na vitanda 60 na kitatoa huduma kamili ya saratani kuanzia utambuzi hadi matibabu," alisema.

Damji alisema kituo hicho kitatoa matibabu ikiwamo upasuaji na mionzi kwa wagonjwa wa saratani kwa watu wa rika zote wakiwamo watoto.

Alisema pamoja na kutoa matibabu, kituo kitatoa mafunzo kupitia timu ya madaktari bingwa wa saratani ili kuwezesha kutoa huduma bora kwa Watanzania na wageni watakaofika kwa ajili ya matibabu.

Pia alisema mara nyingi wagonjwa wa saratani wamekuwa wakifikishwa hospitalini wakiwa katika hatua ya mwisho ya ugonjwa hivyo wengi wao kuishia kupoteza maisha.

Rais wa Kitengo cha Masuala ya Saratani katika Taasisi ya Hospitali ya Apollo, Dinesh Madhavan, alisema ugonjwa wa saratani ni tatizo la kidunia.

Alisema wameamua kushirikiana na Eclipse Group of Africa kujenga kituo cha saratani Tanzania ambacho kitaendeshwa kwa ubora.

"Kwa pamoja tutaimarisha mfumo wa ikolojia wa huduma ya afya Tanzania na kusaidia Watanzania na nchi zingine za jirani katika kupata huduma bora ya saratani bila kusafiri maili kwa ajili ya matibabu nchini India," alisema.

Alisema wataanzisha kituo hicho cha uchunguzi kitakachokuwa na vifaa vya kisasa vya maabara ambavyo vitawezesha utambuzi sahihi wa tatizo.

Naye Agarwal aliipongeza Hospitali ya Apollo na Eclipse Group kwa kuchukua hatua hiyo itakayosaidia Watanzania na nchi nyingine za Afrika kupata huduma bora ya saratani.

Alizipongeza pande zote mbili kwa kufikia hatua hiyo ambayo aliita ni makubaliano chanya katika sehemu ya huduma za afya Tanzania.

Balozi Pradhan, alisema nchi hizo mbili ni washirika wa muda mrefu wa maendeleo na makubaliano kwenye masuala ya afya na dawa yaliyosainiwa mwaka 2002.

Apollo ni kati ya hospitali bora duniani kwa kutoa huduma za juu za matibabu na imegusa maisha ya wagonjwa zaidi ya milioni 150 kutoka zaidi ya nchi 140.

# Jafo ataka mkakati utunzaji mazingira bonde la Mto Nile

**Na Mary Geofrey**

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, Dk. Selemani Jafo, ameitaka Taasisi ya Bonde la Mto Nile (NBI), kutengeneza mikakati endelevu ya kulinda rasilimali za maji za mto huo ili uzidi kuleta maendeleo ya kiuchumi kwa nchi wanachama.

Wito huo aliutoa jana jijini Dar es Salaam, kwa niaba ya Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango, wakati akifungua mikutano ya Baraza la Mawaziri wa Bonde la Mto Nile.

Jafo alisema rasilimali za Mto Nile zinatakiwa kutunzwa kwa sababu zinachangia katika shughuli za kiuchumi kama kilimo, uvuvi, usafiri, biashara na nyinginezo.

"Mnapozungumzia mto Nile mwangalie namna ya kukabiliana na mabadiliko ya tabia kwa kulinda vyanzo vya maji," alisema Jafo.

Alisema jambo hilo liwe endelevu katika mikakati yao kwa sababu ndiyo changamoto kubwa inayoikabili dunia ambayo imechangia kuwapo na ukame uliokithiri na kupungua kwa vina vya maji katika mabonde na mito.

Pia aliwahimiza mawaziri wa nchi wanachama wa bonde la Mto Nile, kuingiza lugha ya Kiswahili itumike kama lugha ya kazi kwenye mijadala au vikao vyao.

Naye Waziri wa Maji ambaye ni Mwenyekiti wa Baraza hilo, Jumaa Aweso, aliwaahidi mawaziri hao kutokuwa kikwazo kwa NBI kuleta maendeleo katika nchi wanachama.

Alisema mpango wa usimamizi wa bonde la Mto Nile unatarajia utakuza utengamano wa shughuli za maendeleo kwa nchi wanachama hivyo ataendeleza ushirikiano na ubia wa maji kwa nchi hizo.

Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji, Dk. Christine Ishengoma, alisema Tanzania ni wanufaika wakubwa wa Bonde la Mto Nile hivyo anategemea ushirikiano zaidi. Mkutano huo ulioanza juzi nchini, lengo ni kuendeleza ushirikiano wa nchi wanachama wa bonde la hilo katika kusimamia na kuendeleza rasilimali za maji.

Mkutano huo umehusisha Baraza la Mawaziri wa Maji wa ENSAP, Baraza la Mawaziri wa Maji Bonde la Mto Nile na Baraza la Mawaziri wa Maji wa Ukanda wa Maziwa Makuu.

HABARI KITAIFA

# DAWASA yaingilia kati uharibifu vyanzo maji

Na Joseph Mwendapole

MAMLAKA ya Majiisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam (DAWASA), imeingilia kati uharibifu wa vyanzo vya maji unaofanywa na wakulima katika mito ya Mgeta, Mngazi, na Dutumi mkoani Morogoro kwa kuwaondoa wakulima wote na mifugo inayosababisha hali hiyo.

DAWASA, ilibaini uharibifu huo baada ya kutembelea na kukagua chanzo cha maji ya Mto Ruvu, katika mito hiyo na kubaini shughuli mbalimbali zinazofanywa na wakulima kwenye vyanzo.

Akielezea uharibifu huo, Mkuu wa Idara ya Mazingira wa DAWASA, Mhandisi Modesta Mushi, alisema wamebaini uwapo wa wakulima wanaozuia maji kwenda kwenye mkondo wake na kuyaelekeza mashambani. Mushi, alisema kwa kiasi kikubwa maji yanapotea katika Kijiji cha Dutumi maarufu kama Kwa Mpina, Mto Dutumi ambako maeneo mawili maji yamezuiwa kutiririka na mifuko ya mchanga.

Alisema, wakulima wamekuwa wakifanya kilimo cha umwagiliaji ndani ya mita 60 za mto katika Kijiji cha Sesenga, Mto Mgeta na wanatoa maji mengi mtoni kwa kuyavuta na mashine bila kuwa na kibali. Mamlaka hiyo, alisema imebaini uharibifu wa tuta lililojengwa kwenye Mto Mgeta katika Kijiji cha Dakawa na kusababisha mto kuhama kutoka njia yake kuu huku akisema kingo za mto zilichimbwa mwaka jana kwa umbali wa kilomita 5.4.

Kwa mujibu wa Mhandisi Mushi, kwenye Mto Mngazi palipojengwa tuta mwaka jana pia pamebomolewa na maji yanapotelea mashambani huku kiasi cha maji yanayorudi kwenye mto kikiwa kidogo sana.

"Tulifika eneo la Dutumi ambako Mto Mgeta na Mngazi inakutana. Maji yaliyopo ni kidogo sana hadi watembea kwa miguu na pikipiki wanapita bila shida," alisema.

Kutokana na uharibifu huo, alisema wanatarajia kufanya kikao cha uhamasishaji na wanakijiji wa Tulo, kutembelea maeneo ya Kongwa na mradi wa umwagiliaji wa Mbaragwe.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Morogoro Vijijini, Rehema Bwasi, alisema mamlaka imefanya jambo la muhimu kukagua na kuona changamoto iko wapi kwenye vyanzo vya maji.

"Uharibifu wa vyanzo vya maji si jambo la kuvumilia kwa kuwa linaleta athari kwa wananchi walio wengi," alieleza Bwasi.

Alisema halmashauri kwa kushirikiana na DAWASA, itahakikisha uharibifu wa vyanzo vya maji ya Mto Ruvu unadhibitiwa na kukomeshwa kwa kushirikiana na ofisi ya Bonde la Wami Ruvu na kuhakikisha watuhimiwa wanaofanya uharibifu wanachukuliwa hatua.


THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

PRESIDENT'S OFFICE

REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT

TANZANIA RURAL AND URBAN ROADS AGENCY (TARURA)

P.O. BOX 11042, DODOMA.

TANZANIA RURAL AND URBAN ROADS AGENCY TARURA Improved Roads For Sustainable Development

REQUEST FOR EXPRESSION OF INTEREST (EOI) (CONSULTING SERVICES – FIRM SELECTION)

**Country:** Tanzania
**Name of Project:** Tanzania Roads to Inclusion and Socioeconomic Opportunities (RISE) Project
**Credit No.:** IDA-68670 - TZ
**Assignment Title:** Provision of Consultancy Services for Feasibility Study, Economic Assessment, Detailed Engineering Design, Preparation of Tender Documents and Construction Supervision for Upgrading of 49km Roads in Ruangwa District and 57km Roads in Handeni District into the Appropriate Sealing Standard.
Reference No. **AE.092/WB-RISE-P164920/276659/2022/23/C/06**

This request for expression of interest follows the General Procurement Notice for this Project that appeared in the United Nations Development Business (UNDB) No. WB-P890351-12/21 of **14th December 2021.**

The Government of the United Republic of Tanzania through Tanzania Rural and Urban Roads Agency (TARURA) and Tanzania National Roads Agency (TANROADS) has received a credit from the International Development Association (IDA) towards the cost of Roads to Inclusion and Social Economic Opportunities (RISE). It is intended that part of the proceeds of the credit will be used to cover eligible payments under the contracts for Consultancy services.

The consulting services ("the Services") intent is to carry out Feasibility Study, Economic assessment, Detailed Engineering Design, Preparation of the Tender Documents and Construction Supervision for Ruangwa – Nangurugai (31km) and Mpiluka – Nandagala (18km) roads in Ruangwa District and Michungwani -Bondo- Kwadoya (19km) and Sindeni – Kwedikwazu (38km) roads in Handeni District. The Feasibility study shall determine the technical and economic feasibility of upgrading the existing gravel/earth road(s) to appropriate sealing standard. Depending on the results of the feasibility study, the Consultant shall undertake detailed engineering design, and preparation of tender documents for International Competitive Bidding (ICB) or National Competitive Bidding (NCB) according to the latest World Bank Standard Procurement Document (SPD). The construction supervision will involve direct on-site supervision of the construction works and supervision during the Defect's Liability Period (DLP).

For Phase I the assignment will include carrying out Feasibility Study, Economic assessment, Detailed Engineering Design and Preparation of the Tender Documents and confidential Cost Estimates for 49km roads in Ruangwa District - Lindi and 57km roads in Handeni District - Tanga. The assignment is expected to be completed within eight (8) months from contract effective date and For Phase II the assignment will include direct on-site supervision of the construction works and supervision during the Defect's Liability Period (DLP) of all roads designed in Phase I. This Phase is expected to be completed forty four (44) months (32 months of Construction supervision and 12 months of DLP) after commencement of Construction contract.

The detailed Terms of Reference (TOR) is attached to this request for Expression of Interest and is also available at TARURA's website www.tarura.go.tz. All requests for clarification should be sent through office email pmurise@tarura.go.tz and the Client will respond to the requested clarifications. The Consultants would be responsible for ensuring that any addenda available on the website is also downloaded and incorporated.

The Chief Executive TARURA, now invites eligible consulting firms ("Consultants") to indicate their interest in providing the above services. Interested consultants should provide information demonstrating that they have the required qualifications and relevant experience to perform the Services. The shortlisting criteria are:

**A. Core business and 10 years in business.**

**B. Relevant similar experience, which should specifically include the below:**
a) Experience of at least two (2) similar assignments completed in the past 5 years. Information to be provided should include name of assignment, name and full contact address of the client, contract value (in equivalent US dollars) and period (dates) of execution of assignment and the role played in the assignment (Lead or JV partner)
b) Demonstration of experience of work in similar conditions.
C. Technical and Managerial Capability of the firm (Provide only the structure of the organization, general qualifications and number of key staff). Do not provide CV of the staff. Experts will not be evaluated at the shortlisting stage).

The attention of interested Consultants is drawn to Section III, paragraphs, 3.14, 3.16, and 3.17 of the World Bank's "Procurement Regulations for IPF Borrowers" Fourth Edition, November 2020 ("Procurement Regulations"), setting forth the World Bank's policy on conflict of interest.

Consultants may associate with other firms to enhance their qualifications but should indicate clearly whether the association is in the form of a joint venture and/or a sub-consultancy. In the case of a joint venture, all the partners in the joint venture shall be jointly and severally liable for the entire contract, if selected. Therefore, each member of JV shall independently meet the requirements of the evaluation criteria. The experience, technical & managerial capability of the Sub-Consultant shall not be evaluated to enhance the qualification of the Lead Firm or JV.

A Consultant will be selected in accordance with the Quality and Cost Based Selection (QCBS) method set out in the Procurement Regulations.

Further information can be obtained at the address below during office hours from 08.00 to 17.00 hours Local time Monday to Friday except public holidays.

Expressions of interest must be delivered in a written form to the address below in person, or by e-mail **pmurise@tarura.go.tz** by **06th September, 2022 14:30** Hours East African Time. The firms that will submit their EOI via e-mail must get confirmation of the receipt of their documents. In case the firm does not receive acknowledgement within two days of after sending the documents via email they should call **+255759348494 or +255745810140** for follow-up.

***The address referred above is:***
***The Secretary, TARURA HQ Tender Board***
***Street Address: Mtaa wa Kazi 41207 Mtumba,***
***Building: TARURA House***
***Address: P.O. Box 11042, Dodoma, Tanzania.***
***Floor/ Room number: Ground Floor/PMU Office***
***City/Town: Mtumba Government City Area***
***Country: United Republic of Tanzania***
***Telephone: +255759348494 or +255673557028***
***Electronic mail address: pmurise@tarura.go.tz***

**CHIEF EXECUTIVE**
**TANZANIA RURAL AND URBAN ROADS AGENCY,**
**P.O. Box 11042, Dodoma.**

21700351

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Tuwekeze utaalamu kwa timu za vijana

**KWA** hali ya kawaida kila klabu inapopambana kuhakikisha inaingiza timu yake kwenye Ligi Kuu inakuwa na malengo.

Zipo timu ambazo malengo yake ni kuwapo tu kwenye Ligi Kuu, hazina mpango wa ubingwa wala kucheza mashindano ya kimataifa. Hili ndilo kundi lenye timu nyingi, kwani humo humo ndimo hupatikana timu zinazoshuka daraja.

Malengo ya aina hii yana maeneo mawili. Moja ni nyenzo kwa maana ya rasilimali uchumi, kwani ili ucheze michuano ya kimataifa unahitaji mamilioni ya fedha kama si mabilioni.

Mfano ni gharama kubwa kushiriki Ligi ya Mabingwa Afrika, vilevile ni faida kwa timu itakayofanikiwa kuwa bingwa kwani inapata fedha nyingi kuliko zile ilizotumia.

Hivyo, kuna sababu za msingi kuingia katika mashindano ukiwa na malengo. Klabu inaweza kutumia nguvu nyingi kuhakikisha inacheza mashindano ya Afrika, lakini ikashindwa kusafiri kwenda kwenye mechi kutokana na kutokuwa na nguvu za kiuchumi.

Kwa Tanzania Bara tunao mfano wa timu za aina hiyo ambazo CAF, hulazimika kuzipiga faini nzito.

Lakini bado timu inayo fursa ya kupigania ubingwa na kuupata, lakini baadaye ikasema haina uwezo kiuchumi kucheza mashindano ya CAF na nafasi yake kupewa timu inayoifuatia baada ya msimamo wa mwisho wa ligi.

Eneo la pili ni la ufundi. Kwa mpira wa miguu, si klabu tu bali hata timu za taifa unapotafuta kocha ni lazima ujue malengo ni nini vinginevyo ni wazi hakitatokea kile ambacho uongozi unakitarajia kuhusiana na matokeo ya uwanjani.

Pia wachezaji wa timu ya Taifa ya wakubwa (Taifa Stars) asilimia kubwa wanatoka katika klabu za ndani. Kwa lugha nyepesi ubora wa wachezaji katika klabu, hasa za Ligi Kuu ndiyo ubora wa timu za taifa, hasa Taifa Stars.

Kwa vile mpira wa miguu ni biashara kubwa na nzuri, bado kuna kila sababu kwa klabu zetu kuwekeza zaidi kwa timu za vijana. Huku faida ni kubwa zaidi kuliko hasara.

Kuwekeza kwa vijana kunatoa fursa kwa wachezaji kupata msingi mzuri wa mpira wa miguu wakiwa bado wadogo.

Lakini kuwekeza huko kwenye vitalu ni biashara nzuri ingawa inahitaji kusubiri na uvumilivu wa kutosha ili kutoa mchezaji au wachezaji wanaoweza kupeleka faida katika klabu husika pia timu ya Taifa.

Kuajiri makocha kwa ajili ya ubingwa hakuna faida kama kuwaajiri kwa ajili ya programu za vijana. Programu za vijana ni uwekezaji na matunda yake yanachukua muda mrefu kuonekana, lakini yakishaonekana yatadumu kwa muda mrefu.


Mpira wa miguu kama ilivyo michezo mingine nguzo yake kuu ni kuwa na wachezaji ambao uwezo wao wa kucheza kwa kasi viwe ni vitu vinavyoongezeka badala ya kupungua. Kwa mantiki hiyo, wanahitajika zaidi wachezaji vijana, kwani hao ndiyo miili yao inaruhusu wawe na kasi uwanjani.

Wachezaji wenye umri mkubwa au wakongwe wanahitajika kwenye timu kwa ajili ya ujuzi na uzoefu wao, lakini si kwa ajili ya kasi. Mpira wa miguu wa kisasa unahitaji kasi uwanjani, hivyo hilo haliwezi kuepukika kwa kocha yeyote.

Wastani wa umri wa wachezaji vijana katika timu unatakiwa kuwa angalau asilimia 70 dhidi ya 30 za wachezaji wakongwe na wazoefu. Nafasi za wakongwe nazo hujazwa na vijana baada ya muda mfupi.

Kwa mafanikio ya muda mfupi makocha wa mataji wanayo fursa katika mpira wa miguu Tanzania. Lakini kwa tulipo hivi sasa kwa hakika tunahitaji zaidi makocha wa maendeleo ya mpira wa miguu kuliko wale wa kuleta mataji.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Adam Fungamwango

# Shindano Ngao ya Jamii sawa, tatizo muda

**HABARI** iliyokuwa gumzo kwa wanamichezo ukiacha kuanza kwa Ligi Kuu Tanzania Bara ni kuanzishwa kwa shindano maalum la ufunguzi wa ligi litakaloshirikisha timu zilizoshika nafasi tatu za juu kwenye msimamo wa ligi na bingwa na Kombe la Shirikisho.

Ni taarifa iliyotolewa na Bodi ya Ligi imeitaka kanuni hiyo kuwa ni ya 19 kuhusu Ngao ya Jamii.

Kwenye taarifa yake, Bodi ya Ligi ikabainisha kuwa endapo bingwa wa Kombe la Shirikisho atakuwa miongoni mwa washindi wa nafasi tatu za juu kwenye msimamo wa Ligi Kuu, timu iliyoshika nafasi ya nne katika msimamo wa ligi itashiriki shindano hilo.

Wadau mbalimbali wa soka wameyapokea kwa mawazo tofauti mabadiliko ya kanuni hiyo.

Wapo wanaoonekana kama wamechanganyikiwa na haelewi ni kwa nini Bodi ya Ligi imeamua hiyo, badala yake wameona ingeachwa vile vile tu.

Binafsi naona ni kama kuboresha timu zetu ambazo mara nyingi hazipati mechi nyingi, hasa za kirafiki.

Ukiangalia shindano hili, utagundua kuwa litachezwa kipindi ambacho ligi inakaribia kuanza, kama vile Simba na Yanga zilivyocheza mechi ya Ngao ya Jamii hivi karibuni.

Naweza kusema shindano hili linaweza kabisa kuzisaidia timu kuangalia wachezaji ambao wamewasajili, pamoja makocha kuangalia mapungufu.

Linaweza kuzifanya timu zikapata muunganiko kabla hata ligi haijaanza.

Pia timu inaweza kuona mapungufu na kocha akaamuru kufanya mabadiliko ya usajili, yaani kuongeza wachezaji wengine baada ya kuona kuwa eneo lina mapungufu kabla kuanza kwa ligi na mechi za kimataifa.

Hizi ni baadhi ya faida zinazoweza kupatikana michuano hiyo itakapoanza msimu huu utakapoamalizika.

Yaani timu nne, tatu za juu kwenye ligi na moja bingwa wa FA zinacheza ligi ndogo kusaka mshindi wa FA, badala ya kanuni ya zamani ambayo inamtaka bingwa wa Ligi Kuu kucheza na wa Kombe la FA.

Na kama bingwa wa Ligi Kuu na huyo huyo ni wa FA, basi atacheza na mshindi wa pili wa Ligi Kuu kama ilivyokuwa kwa Yanga na Simba zilivyocheza.

Hata hivyo, niwape ushauri Bodi ya Ligi ili michuano hiyo iwe ya kufana na isiwe bora liende.

Ukiangalia sana kwa jicho la tatu utaona tatizo la michuano hiyo ni muda. Msimu uliopita Ligi Kuu ilichelewa kumalizika na kama ingeamriwa ichezwe michuano hiyo, basi saa hizi hata ligi ingekuwa haijaanza.

Pamoja na matatizo mengi, ikiwamo ushiriki wa michuano ya kimataifa, ugonjwa wa UVICO na kuipa nafasi timu ya taifa, Taifa Stars kujiandaa, lakini mechi za mchujo zimekuwa nyingi sana ambazo hazina ulazima wowote.

Bodi ya Ligi ingepunguza mechi za mchujo ili kutoa muda wa ligi kumalizika mapema kwa ajili ya kupata muda wa kucheza michuano hiyo mifupi.

Haingii akilini, timu za Ligi Kuu zinacheza mechi za mchujo mechi mbili, halafu inayofungwa inakwenda kucheza tena mechi mbili za mchujo na timu za Ligi ya Championship.

Haya ni matumizi mabaya ya muda. Ili michuano hiyo ipate nafasi na ligi ianze mapema, nashauri kuwa timu itakayoshika nafasi ya 13 na 14 kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara zikicheza mechi ya mchujo nyumbani na uganini, itakayopata matokeo mabaya ya jumla ishike moja kwa moja daraja ili tusipoteze muda.

Na timu inayoshika nafasi ya tatu na ya nne kwenye Ligi Kuu zicheze na itakayoshinda ipande moja kwa moja Ligi Kuu badala ya kuwa na mlolongo wa mechi nyingi ambazo ukija kuziunganisha na michuano ya Ngao ya Jamii ligi inaweza kuchelewa kuanza bila sababu maalum.

Vinginevyo inaweza kuwafanya hata wachezaji wakose muda wa kupumzika ligi itakapomalizika, kwani zipo timu zinakwenda kucheza mchujo na hapo hapo zianze shindano hilo.

# Shaka aonya watumishi unyanyasaji wa kingono

**Na Mwandishi Wetu,** SIKONGE

CHAMA Cha Mapinduzi (CCM), kimeonya na kukemea tabia ya udhalilishaji kingono inayodaiwa kufanywa na baadhi ya watumishi waliopewa dhamana katika halmashauri mbalimbali ikiwamo ya Sikonge.

Onyo hilo lilitolewa juzi na Katibu wa Halmashauri Kuu ya Taifa (NEC) Itikadi na Uenezi, Shaka Hamdu Shaka, wilayani hapa katika ziara ya kukagua utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM na uhai wa chama mkoani Tabora.

Shaka, alisema hayo baada ya kuwapo malalamiko juu ya kushamiri kwa vitendo hivyo wakati wa ziara yake wilayani Kaliua na Sikonge na kuonya kubainisha kuwa chama hakiungi mkono udhalilishaji wowote na inafuatilia hatua kwa hatua jambo hilo.

"Nataka niseme hili la udhalilishaji kwa wanawake kingono, nimelikuta Kaliua na lipo Sikonge. Hata kwenye maeneo mengine kwa watumishi wa umma. Ujumbe umefika, wenye hiyo tabia waache.

"Waache kuwadhalilisha dada zetu, waache kuwadhalilisha mama zetu, waache kuwadhalilisha ndugu zetu wa kike hapa Sikonge. Hiyo tabia imeshamiri kwa sababu tu kuna mtu ana dhamana, ana fursa ya kuwasaidia wengine.

"Hamwasaidii mama zetu, hamsaidii dada zetu mpaka muwadhalilishe kingono? Chama kinafuatilia kwa karibu sana na hatuturahusu udhalilishaji wa aina yoyote kwa wanawake ndani ya nchi hii. Wanawake hawa wana uwezo mkubwa sana katika kufungua fursa za maendeleo katika taifa letu.

"Wakithubutu kinamama wanaweza, hatuwezi kuacha uthubutu wao kwa sababu tu sisi akina baba baadhi yetu tunashindwa kuzuia hisia zetu, tena sio kushindwa kuzuia hisia zetu ila hatuna adabu tu, ni utovu wa adabu tuliokuwa nao," alisema.




Mkurugenzi Mtendaji wa Global Education Link (GEL), Abdulmalik Mollel (katikati), akizungumza na waandishi wa habari, jijini Dar es Salaam juzi, kuhusu mahafali ya tatu kwa wanafunzi waliosoma nje ya nchi yanayotarajiwa kufanyika Mlimani City, kesho. Kushoto ni Mkurugenzi wa Mambo ya Nje wa GEL, Robert Kibona. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# Walia mwekezaji kufunga barabara

**Na Faustine Feliciane**

WANANCHI na baadhi ya wawekezaji wa hoteli katika Kata ya Kimbiji, Kigamboni mkoani Dar es Salaam, wameiomba serikali kuiamuru kampuni ya ASM (T) LTD kutenga eneo la barabara ili kufika katika maeneo yao.

Ombi hilo linatokana na ASM inayomiliki viwanja viwili vinavyotazamana katika barabara inayoelekea kwenye ufukwe wa bahari, kushinda kesi dhidi ya Manispaa ya Kigamboni na Mwanasheria Mkuu wa Serikali, aliyoifungua mwaka 2019 kupinga matumizi ya barabara hiyo.

Akizungumza na waandishi wa habari, Mwenyekiti wa Serikali ya Mtaa wa Mikenge, Kata ya Kimbiji, Lameck Mayala, alisema hawana tatizo na mwekezaji huyo kushinda kesi yake, lakini wanamtaka kutumia busara kutenga eneo la barabara ili kuwasaidia wananchi ambao wengi wao ni wavuvi kufika baharini kufanya shughuli zao.

"Tunafahamu ameshinda kesi yake. Sisi hatuna tatizo na jambo hilo lakini pia tunafahamu hukumu iliyotolewa na mahakama, imetoa nafasi ya pande zote kukaa na kutafuta suluhisho la barabara kwa sababu mbele ya eneo la ASM kuna wawekezaji wengine waliojenga hoteli zao na vijana wetu wengi wamepata ajira huko.

"Pia wananchi wengi wa huku ni wavuvi na wanaitegemea barabara hiyo kufika kwenye maeneo yao ya kazi, hivyo tunaomba halmashauri kama ilivyoagizwa kukutana na mwekezaji na kutatua kero hii. Tunataka eneo la barabara kama hii iliyoko sasa," alisema Mayala.

Mwenyekiti huyo alisema tayari mwekezaji huyo ameshajenga ukuta kuifunga barabara hiyo inayoingia kwenye maeneo ya hoteli na ufukweni.

Mmoja ya wawekezaji wa hoteli katika eneo hilo, Vidate Msoka, anayemiliki Hoteli ya Light House Beach Lodge ambayo kwa sasa haifikiki kutokana na kufungwa kwa barabara hiyo, alisema kwa sasa hakuna biashara inayofanyika kwa kuwa wageni wanaofanya 'booking' kufika hotelini kwake au hoteli za jirani wanashindwa kufika kutokana na kufungwa kwa barabara hiyo.

"Yaani hata kwa bahati mbaya likitokea janga la moto huku sijui tutafanya nini. Kwa sasa magari hayafiki. Unadhani tutauzima vipi? Tunaomba mwekezaji mwenzetu atoe ushirikiano kwa halmashauri kutatua kero hii. Tunafahamu anaitwa halmashauri lakini amekuwa hatoi ushirikiano," alisema Msoka.

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Kigamboni, Erasto Kiwale, alipoulizwa juu ya sakata hilo, alikiri mwekezaji kushinda kesi na kwa sasa anafuatilia kuona watatatua vipi kero hiyo. "Bado tunafanyia kazi suala hili, mimi ni mtendaji na hii ndiyo kazi yangu. Tunafuatilia kuona tunaweka sawa kila kitu kwa hiyo itoshe kusema bado tunafanyia kazi suala hili," alisema Kiwele alipoulizwa baada ya Mkuu wa Wilaya hiyo, Fatuma Nyangasa kusema jambo hilo liko kwenye halmashauri.

Mkurugenzi Mtendaji wa ASM (T) LTD, Abdallah Salim Mohamed, alipotafutwa na gazeti hili kwa njia ya simu kutoa ufafanuzi, aliomba kuandikiwa ujumbe mfupi wa maandishi lakini hata alipoandikiwa hakutoa maelezo yoyote na alipopigiwa tena, hakupokea.

# Mkuu wa mkoa ahimiza weledi, uaminifu sensa

**Na Friday Simbaya,** IRINGA

ZIKUWA zimebakia siku chache kufanyika kwa sensa ya watu na makazi Agosti 23, mwaka huu, Mkuu wa Mkoa wa Iringa, Halima Dendego, amewataka makarani mkoani hapa kufanya kazi kwa weledi na uaminifu.

Akizungumza jana na makarani na waratibu wa sensa katika vituo mbalimbali vya mafunzo wa sensa alipokwenda kuwasalimia na kuwatia moyo, Dendego aliwataka makarani wakafanye kazi hiyo kwa uadilifu.

Dendego pia alitumia nafasi hiyo kujitambulisha kwa makarani na waratibu wa sensa kama mkuu wa mkoa baada ya kuteuliwa na Rais Samia Suluhu Hassan hivu karibuni.

Aliwahakikishia kwamba kazi ya serikali ni kuwawezesha ili wafike na kufanya kazi ya kuhesabu kwa usalama kwa masalahi mapana ya maendeleo.

Sensa ya watu na makazi, kwa mujibu wa Dendego, ni muhimu kwa masilahi mapana ya maendeleo na kwamba itasaidia serikali kujua idadi ya watu wake ili kupanga shughuli za maendeleo kulingana na takwimu halisi.

"Tukihesabiwa na tukihesabu na kujuana kwa shughuli zetu itasaidia serikali na wadau mbalimbali wa maendeleo kuweza kupanga na kutoa huduma kulingana na mahitaji," alisema.

Mratibu wa Sensa ya Watu na Makazi Mkoa wa Iringa, Peter Milinga, alisema baada ya walimu wa makarani kumaliza mafunzo, wako tayari kwenda kufanya kazi ya kuhesabu watu na makazi.

Alisema kwa mafunzo waliyopata makarani hao, watakwenda kufanya kazi hiyo kwa usahihi na uhakika na hawana shaka na hilo.

Milinga alisema matarajio ya sensa ni kupata taarifa zilizo bora, sahihi na kwa weledi. Makarani 4,696 watatumika kufanya kazi ya sensa kwa mkoa wa Iringa.z

Mratibu huyo amewaomba wana Iringa na wananchi kwa ujumla kutunza taarifa muhimu ambazo makarani watazitaka kama vile kitambulisho cha taifa (NIDA), pasipoti, leseni ya udereva na kadi ya mpigakura.

"Kama mkuu wa kaya atakuwapo nyumbani lazima aache taarifa muhimu kama vile kitambulisho cha NIDA, namba ya simu ya mkuu wa kaya," alisema.

Milinga aliwataka pia wenye hoteli na nyumba za kulala wageni kuhakikisha wanaweka taarifa za wageni watakaolala usiku wa kuamkia siku ya sensa ili makarani watakapopita, wapate taarifa sahihi.

"Safari hii taarifa zitaanza kukusanywa tangu kitongoji kwa sababu ya matumizi ya teknolojia. Kwa hiyo mafunzo haya ni muhimu sana," alisema.

# Mafunzo kabambe kukuza sekta utalii

**Na Julieth Mkireri**

CHUO cha Taifa cha Utalii (NCT) kinatarajia kuanza kutoa mafunzo kwa zaidi ya wadau 5,000 walio katika mnyororo wa utalii ili kuboresha utoaji wa huduma lengo ikiwa ni kukuza sekta hiyo.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa NCT, Dk. Shogo Mlozi, aliyasema hayo jana chuoni hapo, Dar es Salaam, alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari akizungumzia uzinduzi wa mpango huo.

Alisema kupitia mpango huo, Tanzania itaendelea kutembelewa na watalii zaidi na kufikia malengo ya watalii milion tano kwa mwaka ifikapo mwaka 2025.

Dk. Mlozi, alisema watakaonufaika na mafunzo hayo ni maofisa uhamiaji, waandishi wa habari, maofisa polisi, waendeshaji wa vyombo vya usafiri, wauza vyakula na wadau wengine.

Alisema kupitia mpango huo, chuo kimekusudia kufikia idadi hiyo ya wadau kutoka katika mikoa ya Dar es Salam, Zanzibar, Arusha, Kilimanjaro, Mwanza na mikoa mingine kuzingatia kuwa ni maeneo yaliyo na huduma nyingi za kitalii.

Mpango wa mwanzo, alisema chuo kinatarajia kutoa mafunzo kwa maofisa uhamiaji 700, ambao ndio hukutana na wageni wengi wenye mahitaji mbalimbali wanaotoka na kuingia nchini kwa madhumuni tofauti ikiwamo shughuli za utalii.

"Ifahamike kuwa mafunzo haya ni mwendelezo wa jitihada mbalimbali zinazochukuliwa na serikali, wadau na viongozi wengine hususani Rais Samia Suluhu Hassan, kuinua sekta ya utalii," alisema.

Kwa mujibu wa Dk. Mlozi, chuo kimejipanga kuendeleza programu ya The Royal Tour kwa kuanza kutoa mafunzo ya lugha za kigeni kama Kichina na Kiitaliano ambapo pia wanafunzi wataruhusiwa kuchagua kujifunza lugha za Kijerumani.

Chuo hicho pia kinatarajia kuanza kufungua matawi katika Nyanda za Juu Kusini mwaka huu kwa kuwa yako maeneo ya utalii ambayo wageni wanaweza kuyatembelea.

Waziri wa Wizara ya Maliasili na Utalii, Pindi Chana, anatarajia kuwa mgeni rasmi kwenye uzinduzi wa mafunzo hayo yanayozinduliwa leo.

# Pinda asisitiza midahalo hoja zenye tija

**Na Halfani Chusi**

NAIBU Waziri wa Katiba na Sheria, Geofrey Pinda, alisema serikali itaendelea kufanyia kazi hoja na mapendekezo yanayoibuliwa katika midahalo mbalimbali inayohusu masuala ya sheria kwa lengo la kuisaidia serikali katika kutimiza majukumu yake.

Pinda, aliyasema hayo juzi wakati wa kongamano la kutimiza miaka 30 ya mfumo wa demokrasia ya vyama vingi lililofanyika jijini Dar es Salaam na kuhudhuriwa na wanafunzi wa vyuo vikuu, wanasheria, mawakili wa kujitegemea na wa serikali, wafuasi wa vyama vya siasa pamoja na wadau wengine kutoka taasisi mbalimbali.

Alisema, serikali itakuwa macho katika kupokea ushauri unaopatikana kutoka katika majukwaa mbalimbali huku akibainisha kuwa serikali hutumia hoja zinazoibuliwa kuunda kitu fulani.

"Nimefurahi kualikwa katika kongomano hili kwa sababu mambo yatakayojadiliwa hapa yakitufikia sisi tutaenda kuyatumia katika kujenga nchi yetu, hivyo wadau mliopo humu changieni hoja muwezavyo ili kuona ni sehemu gani ina upungufu tufanyie kazi mapema iwezekenavyo," alisema.

Rais wa Chama cha Wanasheria wa Tanganyika (TLS), Dk. Edward Hoseah, alisema Watanzania wanatakiwa kuitumia mahakama kupata haki badala ya kulalamika pindi wanapobaini uwapo wa shida katika demokrasia.

"Mahakamani ndiyo sehemu pekee ya kupata haki. Watanzania wengi ni watu wa kulalamika, lakini si kufika kwenye vyombo vya sheria, hivyo niwaombe Watanzania wenzangu kutokuogopa kufika mahakamani. Kwa mfano, uchaguzi mkuu uliopita, tulikuwa tunasikia malalamiko mitaani lakini hatukuona hata shtaka moja likifikishwa mahakamani, sjui shida iko wapi?" alihoji.

Katibu Mkuu wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), John Mnyika, alirejea hitilafu alizoziona katika kipindi cha mika 30 ya demokrasia ya vyama vingi ikiwa ni pamoja na kunyimwa haki ya kufanya mikutano ya kampeni kwa vyama vya upinzani, uchaguzi usio wa uhuru na haki, kuibiwa kura wakati wa uchaguzi kushambuliwa na kuonewa kwa baadhi wa wafuasi wa chama hicho akitolea mfano kitendo cha kupigwa risasi aliyekuwa Mbunge wa Singida Mashariki, Tundu Lisu.

Mkurugenzi Mtendaji Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), Anna Henga, aliiomba serikali kuridhia mkataba wa Afrika wa demokrasia na uchaguzi wa mwaka 2007, pamoja na kuvipa vyama uhuru wa kufanya mikutao ya hadhara kwa muujibu wa katiba ambayo imefungiwa tangu mwaka 2016.



Katibu wa CCM wa Kata ya Manzese Dar es Salaam, Ramadhan Kidoga akipongezwa na aliyewahi kuwa Waziri wa Maliasili na Utalii katika serikali ya awamu ya nne, Shamsa Mwangunga (kushoto), baada ya kufanikiwa kutetea nafasi hiyo, kwenye uchaguzi uliofanyika hivi karibuni. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Exim yakumbuka waliotumikia miaka 25

**Na Mwandishi Wetu**

BENKI ya Exim Tanzania, imeadhimisha miaka 25 tangu kuanzishwa kwake kwa kutambua jitihada na mchango wa wafanyakazi wa benki hiyo kufanikisha ustawi wake.

Hafla hiyo ililenga kuwapongeza watumishi wa benki hiyo waliohudumu kwa zaidi ya miaka 25 ilipoanzishwa.

"Benki ya Exim imejitolea kwa dhamira yetu ya dhati kuwaweka wadau wetu muhimu wakiwamo wafanyakazi na wateja mbele," alisema Jaffari Matundu, Ofisa Mtendaji Mkuu wa benki hiyo.

"Wafanyakazi wetu ndio wanaosimamia dira yetu ya kila siku wakitoa huduma ya kipekee kwa wateja wetu. Tukio hili linatoa fursa kwetu kutambua juhudi zao za pamoja, na kusherehekea mafanikio ambayo yasingewezekana bila wao," aliongeza.

Matundu, alisema maadhimisho hayo yanahusisha matawi yote ya benki nchi nzima na yatahusisha mpango wa benki hiyo katika kusaidia jamii kwa namna mbalimbali.

Kwa mujibu wa Matundu, benki hiyo imejipanga zaidi kuendelea kuwapa wateja wake bidhaa na huduma za kibunifu huku ikijiweka katika nafasi ya ushindani mkubwa katika ukanda wa Afrika Mashariki.

"Ili kuendelea kufikia malengo yetu, miaka ijayo tunahitaji kuwa na uvumbuzi zaidi, teknolojia salama na yenye ufanisi, huduma bora kwa wateja na zaidi ya yote, ushirikiano mkubwa na msaada wa wateja wetu, washirika wa biashara, mamlaka mbalimbali na wadau wengine wote," alisema.

Akizungumza katika hafla hiyo, Mkuu wa Rasilimali Watu wa Exim, Fredrick Kanga, aliwashukuru wafanyakazi hao kwa mchango wao katika ukuaji wa benki hiyo huku akibainisha kuwa uongozi unaheshimu na kutambua umuhimu wa kila mfanyakazi katika kuleta maendeleo ya benki hiyo.



# TIC yazidi kuvutia uwekezaji

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WIZARA ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji kupitia Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC), inaendelea kutambua fursa za uwekezaji, kuzitangaza na kusajili miradi ili kusaidia upatikanaji wa vibali na leseni kwa wawekezaji.

Kaimu Meneja wa TIC Kanda ya Kati, Juma Nzima, alibainisha hayo juzi jijini hapo alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari kuhusu mikakati ya wizara hiyo katika sekta ya uwekezaji.

Kadhalika, alisema ili kufanikisha uwekezaji nchini kituo hicho kinasimamia upatikanaji wa ardhi kwa wawekezaji na kutatua vikwazo vya uwekezaji.

Alisema TIC, inawavutia wawekezaji wa ndani na nje ya nchi ili kukuza sekta binafsi na hatimaye kuinua uchumi wa taifa pamoja na kuishauri serikali kuhusu masuala yanayohusu uwekezaji nchini.

Nzima, alisema kituo hicho kimejikita katika kutekeleza Dira ya Maendeleo ya Taifa ambayo inapanga Tanzania kuwa ya viwanda ifikapo 2025.

"Kazi zinazofanywa na kituo hiki ni kuhakikisha tunafanikisha kufanya tafiti zenye lengo la kutangaza fursa za uwekezaji kwa wajasiriamali na kufanikisha utekelezaji wa miradi ya uwekezaji inayoanzishwa," alisema.

Kuhusu taratibu mbalimbali za huduma kwa wawekezaji alisema, ili wawekezaji kuanzisha miradi mbalimbali nchini wanahitaji kupata vibali na leseni kupitia kitengo cha huduma za mahala pamoja na utaratibu wa kupata cheti cha uwekezaji unazingatia uthibitisho wa fedha za kutosha za kutekeleza miradi.

"Kuna masharti pia katika utaratibu wa usajili wa kampuni za nje. Mwekezaji atatakiwa kuwasilisha nyaraka tatu kutoka kwenye kampuni mama ambazo zimethibitishwa na mwanasheria wao, ambazo ni katiba ya kampuni, cheti cha usajili wa kampuni na taarifa za ukaguzi wa hesabu," alisema.

Hata hivyo, alisema kupitia matukio mbalimbali ya kitaifa wataendelea kutoa elimu kwa wananchi kuhusu utaratibu wa kuomba leseni ya biashara kwa ajili ya uwekezaji ambapo mwombaji ataambatanisha nakala ya cheti cha kampuni kwa wale wenye kampuni au cheti cha usajili kwa wenye majina ya kibiashara.




Mjasiriamali Mwita Marwa ambaye ni mlemavu wa miguu akichomelea mabomba kwa ajili ya kuitengeneza baiskeli inayotumiwa na watu wenye ulemavu kwenye karakana yake, katika stendi ya Sabasaba, jijini Dodoma juzi. **PICHA: PETER MKWAVILA**

## TFRA yawatoa hofu wakulima

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

MAMLAKA ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA), imewatoa hofu wakulima wa mkoa wa Dodoma, na maeneo mengine ambayo vituo vya uwakala wa kusambaza mbolea ya ruzuku havijatangazwa, hivyo vitatangazwa kwenye awamu zingine kutokana na maombi yaliyowasilishwa.

Hivi karibuni, mamlaka ilitangaza vituo vya mawakala wa mbolea hiyo kwenye baadhi ya mikoa huku mikoa mingine ikiwa haina vituo.

Miongoni mwa mikoa yenye vituo ni Dar es Salaam, Iringa, Kigoma, Kilimanjaro, Mbeya, Njombe, Ruvuma, Shinyanga, Songwe, Katavi, Manyara, Mwanza, Tabora, Arusha, Geita, Simiyu na Tanga.

Kutokana na hali hiyo, Nipashe ilimtafuta Kaimu Meneja wa Uhusiano na Mawasiliano kwa Umma wa TFRA, Matrida Kasanga, ili kujua mikoa ambayo haijatangaziwa vituo, aliwataka watoe hofu wakulima kuwa tangazo la vituo lililotolewa jana ni la awamu ya kwanza na wataendelea kutoa kwa awamu vituo hivyo kulingana na maombi.

"Naomba wakazi wa Dodoma na maeneo mengine msiwe na wasiwasi, orodha ya vituo hivyo imetolewa kulingana na walivyoomba katika mfumo," alisema Kasanga.

Alisema, bado mamlaka hiyo inaendelea kuandaa tolea lingine ambalo litabainisha kila wakala na kituo chake pamoja na kampuni ambazo zitahusika kwa ajili ya kusambaza mbolea ya ruzuku kwa wananchi wa maeneo mbalimbali.

Pia, alisisitiza wakulima waendelee kujisajili kwenye mfumo uliotolewa na serikali ili iwe rahisi kwao kupata mbolea ya ruzuku.

Alisema, kujisajili kwa wingi kutawapa nafasi wao ya kuingia kwenye mfumo wa kupata mbolea hiyo kabla ya msimu wa kilimo kuanza.

"Waende serikali za vijiji vyao kujisajili kwa ajili ya kuingizwa kwenye mpango wa utoaji mbolea ya ruzuku," alisema.

# Kikwazo ufugaji kuku kisasa chaanikwa

**Na Valentine Oforo,** DODOMA

WAFUGAJI wengi wa kuku wanashindwa kufuga kitaalamu kutokana na gharama kubwa hususani upatikanaji wa vizimba vya kisasa.

Kutokana na hali hiyo, Kikundi cha Vijana Wajasiriamali cha Tusumuke (TYEG), cha jijini Dodoma, kinatekeleza mradi wa uzalishaji na uuzaji wa vizimba vya kuku vya kienyeji ili kuwasaidia wafugaji hao kupunguza gharama katika kusimamia miradi yao.

Akizungumza na Nipashe, Mwenyekiti wa TYEG, Christopher Dioniz, alisema vizimba vingi huagizwa kutoka nje na kuuzwa kwa gharama kubwa.

Dionjiz, alisema kikundi hicho kinazalisha vizimba vya kienyeji vyenye uimara mkubwa na uwezo wa kuhifadhi kuku wasiopungua 100. Alisema, kwa sasa kikundi kinauza vizimba (mabanda) ya kuku kwa Sh. 450,000, kiwango ambacho ni nafuu ukulinganisha na vizimba vya kisasa vinavyoagizwa kutoka nje ya nchi, ambavyo vinauzwa kwa Sh. 750,000. "Maono ya mradi huu ni kuwasaidia wafugaji wa kuku hapa nchini ili kupunguza gharama kubwa ambazo wanakabiliana nazo katika kushughulikia miradi ya ufugaji wa kuku, husasani katika kununua vizimba. Tunashukuru Mungu kwani mpaka sasa tumefanikiwa kuuza hivi vizimba kwa wafugaji katika mikoa sita," alisema Dioniz.

Mbali na kuuza vizimba hivyo, alisema kuwa kikundi hicho pia kinatoa mafunzo kwa wafugaji juu ya namna bora ya kutengeneza vizimba hivyo, hatua ambayo hadi sasa imeweza kutoa fursa ya ajira kwa takribani vijana 12 katika mikoa tofauti.

Katika mwendeleo wa jitihada za kusaidia kupunguza gharama za kufuga kuku miongoni mwa wafugaji wa Tanzania, Dioniz alisema kikundi hicho kwa kushirikiana na Wizara ya Mifugo kimeagiza makinikia kutoka Uholanzi kwa ajili ya uzalishaji wa chakula cha kuku.

"Kwa kutumia makinikia hayo, yanayojulikana kama 'Koudijs concentrate' kikundi hiki kwa sasa kinaweza kuzalisha chakula cha kuku chenye virutubisho vingi kupitia mchanganyiko wa mahindi, chokaa na pumba, na kukiuza kwa wafugaji kwa bei nafuu ya kati ya Sh. 1,100 na 1,500," alisema.





# Othman asifu kikosi kazi cha Samia

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MAKAMU wa kwanza wa Rais Zanzibar, Othman Masoud Othman, amekutana na kikosi kazi cha Rais Samia kuhusu masuala yanayohusu demokrasia ya vyama vingi vya siasa.

Othman alipongeza hatua hiyo na kupata fursa ya kutoa maoni yake pamoja na kujibu masuala aliyoulizwa na kikosi kazi hicho.

Akizungumza jana na waandishi wa habari mjini Zanzibar baada ya kumaliza kutoa maoni yake, Othman aliwataka wananchi na viongozi kutumia fursa ya kuwapo kwa kikosi kazi hicho kutoa maoni yatakayosaidia kujenga mustakabali wa nchi yenye kuzingatia demokrasia, utawala bora na kukuza uchumi.

Kikosi hicho, alisema kimeundwa kwa lengo la kukaribisha maoni mbalimbali ya wananchi wakiwamo viongozi kuhusu muundo wa mifumo gani mwafaka zaidi katika kuendesha pande mbili za Muungano pamoja na kisiasa na kiuchumi.

Aliwataka wananchi kuitumia fursa hiyo kutoa maoni yenye kujenga mustakabali wa taifa na kuacha tabia ya kubeza shughuli za kikosi kazi hicho.

Kuhusu uendeshaji wa Muungano, Othman alisema kuna kasoro nyingi ambazo hazijafanyiwa kazi, hivyo zinahitaji marekebisho makubwa huku akiitaja Tume ya Pamoja na Fedha ambayo ilianzishwa chini ya Katiba ya Muungano mwaka 1984. Tume hiyo ilikusudiwa kusimamia uhusiano ya kifedha baina ya pande mbili za Muungano na kuwapo kwa akaunti ya pamoja ya fedha.

Alisema Sheria ya Tume ya Pamoja ya Fedha ilitungwa mwaka 1996 na kuanza kufanya kazi Agosti, 2006 kwa kuwasilisha mapendekezo mbalimbali kwa pande mbili za Muungano.

"Tume kwa kadri siku zinavyokwenda inaonekana kupoteza mwelekeo na kutoonekana umuhimu wake tena licha ya kuwapo kwa mujibu wa Katiba. Kwa mfano, ni muda mrefu sasa tume hiyo haina mwenyekiti wala makamu mwenyekiti au makamishna," alisema.

Aidha, Othman alisisitiza kuwapo kwa Tume Huru ya Uchaguzi ambayo itafanya kazi kwa mujibu wa Katiba na sheria bila kuingiliwa na mtu yetote ikiwamo kuendesha na kusimamia uchaguzi huru.

Uchaguzi, alisema ndio utaratibu unaotumika kwa mujibu wa Katiba na sheria kuweka viongozi watakaoendesha nchi, hivyo ni muhimu kuwapo kwa makamishna huru watakaochaguliwa kwa mujibu wa vigezo na sifa ikiwamo kuomba nafasi hizo.

"Moja ya maeneo ambayo tunahitaji kuliimarisha zaidi kwa kuendesha na kusimamia uchaguzi huru na haki ni tume ya uchaguzi itakayokuwa na makamishna waliotuliwa kulingana na sifa na vigezo vya uadilifu na kuheshimika katika jamii," alisema.



Mwenyekiti wa Taasisi ya Nuru ambaye ni Mke wa Makamu wa Kwanza wa Rais Zanzibar, Zainab Kombo Shaib, akizungumza na wazazi na walezi wa watoto yatima katika Kijiji cha Kitambuu, Shehia ya Mchangamdogo, Mkoa wa Kaskazini Pemba, baada ya kugawa misaada ya vyakula, sabuni na huduma za kujikimu kwa watoto yatima, wenye mahitaji maalum na mazingira magumu. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wavuvi waombwa subira upatikanaji boti

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WAVUVI wa Malindi, Mjini Unguja, wametakiwa kuwa na subira ya upatikanaji wa boti za uvuvi kutokana na idadi kubwa ya boti zinazohitajika kutengenezwa kutokana na kampuni chache za utengenezaji wa zana hizo.

Mwenyekiti wa Kamati ya Uchumi ya Baraza la Wawakilishi (BLW), Sabiha Filfil Thani, alisema hayo jana katika ziara ya mwendelezo wa kuonana na wavuvi na kuangalia miradi mbalimbali ikiwamo ujenzi wa soko jipya la Malindi.

"Tumeliona jengo la kiwango cha juu na tunaishukuru serikali ya Japan kwa kutupatia msaada ambao utasaidia taifa katika kuwawezesha wavuvi kupitia soko hili la Malindi," alisema.

Sabiha alisema Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi inajitahidi kuwa karibu na kampuni zilizopewa dhamana ya utengezaji wa boti ili kujua ubora wa vifaa vinavyotumika pamoja na kuzifanyia majaribio boti za uvuvi.

Alisema serikali kupitia wizara hiyo, iko katika kufanikisha upatikanaji wa boti kubwa zinazochukua idadi kubwa ya manahodha kwa ajili ya uvuvi wa bahari kuu ili kujikwamua kimaisha.

Naye Katibu Mkuu wa Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi, Dk. Aboud Suleiman Jumbe, alisema zaidi ya boti 350 za mwani na boti 100 za uvuvi tayari zimekamilika na ziko tayari kwa ajili ya uwasilishwaji huku shughuli za utengezaji wa boti zingine ukiendelea . Dk. Aboud alisema serikali ina mpango mpya wa utengezaji wa boti kubwa ambazo zitakuwa na uwezo wa kuchukua manahodha 80 zinazotarajiwa kuvua katika uvuvi wa bahari kuu.

Alisema wizara inaendelea na mchakato wa utoaji wa elimu kwa wavuvi ambao wako tayari kwa ajili ya kupatiwa fursa ya mikopo nafuu ya uvuvi na mazao ya bahari.

Wavuvi kwa upande wao walisema ni faraja kwao baada ya kushirikishwa katika kila hatua na wako tayari kutoa maoni kwa taasisi husika baada ya kuangalia boti za uvuvi kwa ajili ya mkandarasi kuendelea na maboresho zaidi na ikiwa kinastahiki kiendelee na shughuli za uvuvi.

Mmoja wa wavuvi hao, Khamis Ali, aliomba serikali kuwapatia boti za uwokozi pindi yanapotokea majanga katika shughuli zao za uvuvi ili iwe rahisi kutatua matatizo yanayowakabili baharini.

## SMZ yaahidi kuwalinda, kuenzi wapiganaji wake

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

SERIKALI ya Zanzibar imesema itaendelea kuwalinda, kuwaheshimu, kuwaenzi na kuboresha maslahi yanayowahusu wapiganaji wa vikosi vyake ili kuendelea kufanya kazi kwa uadilifu.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalumu za SMZ, Masoud Ali Mohamed, alisema hayo jana katika sherehe za upandishaji wa bendera ya Kikosi cha Valantia (KVZ) iliyofanyika jana katika kambi ya Mtoni, mkoa wa Mjini Magharibi.

Alisema KVZ ni miongoni mwa vikosi vyenye historia ndefu ndani ya Zanzibar na Tanzania kwa ujumla kutokana na kutoa mchango mkubwa wa kuanzishwa kwa taasisi mbalimbali za ulinzi likiwamo Jeshi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ).

Pia alisema kikosi hicho kwa mujibu wa malengo ya kuanzishwa kwake, kinategemewa katika ulinzi wa nchi hasa ikizingatiwa kuwa ni kikosi cha ardhini.

Alisema wanapopandisha bendera ya kikosi hicho ni wajibu wao kuendelea kulinda misingi ya Mapinduzi ya Zanzibar na kuwalinda wananchi na mali zao pamoja na viongozi wao kwa ajili ya kuiletea tija nchi yao.

Pia alisema alama hiyo ya upandishwaji wa bendera inapaswa kuongeza ari, chachu, morali wakati wowote wa kuwajibika katika kazi.

"Bendera hiyo inapopepea ndani na nje ya kambi zetu, ikainue ari ya kutimiza wajibu wetu na tutakuwa hatuitendei haki wakati bendera hiyo inapopeperushwa na kushushwa unapoiona usiiheshimu," alisema.

Naye Kamanda wa Kikosi hicho, Luteni Kanali Said Shamuhuna, alisema hatua ya kupandisha bendera hiyo, itakipa heshima kubwa kikosi hicho ambacho kimeisaidia nchi katika ukombozi wake.

Alisema akiwa kamanda wa kikosi hicho, ataendelea kuona bendera ya kikosi hicho inaheshimika ndani na nje ya kambi yao.



GIGI MONEY

UKURASA 12

Nipashe
MWANGA WA JAMII

BT

JUMAMOSI AGOSTI 20, 2022



# BARNABA BOY

## Umbo dogo, mapigo ya kibabe

HIVI karibuni mwanamuziki nyota wa Bongo Fleva, Elias Barnaba, maarufu kama Barnaba amezindua albam yake mpya 'Love Sounds Different' kwa mafanikio.

Katika ukumbi wa Mlimani City, Barnaba ameweza kuonyesha umwamba wake katika muziki kwa kuimba nyimbo na wanamuziki mbalimbali kwa ubora wa hali ya juu.

Jina la Barnaba limekuwa kubwa ukilinganisha na umbo lake. Hata hivyo msanii huyo anazidi kuonyesha kwamba umbo si kitu katika mafanikio, bali kipaji na namna ya kukitumia ipasavyo.

Mkali huyo wa nyimbo mbalimbali zinazotamba katika ukanda wa Afrika Mashariki, anajivunia kwa kuwa na jina imara lisiloshuka kisanaa,

hata katika ukuaji wa muziki wa Bongo Fleva, Barnaba amechangia kwa kiasi kikubwa kutokana na umahiri wake wa kupiga ala na kutunga nyimbo tamu kwake yeye binafsi na wasanii wengine.

Akianzia wimbo wake wa kwanza "Baby I Love You" alioutoa mwaka 2007, hakuwahi kushuka na badala yake nyota yake iliendelea kung'aa hadi sasa.

Pamoja na mafanikio hayo, Barnaba hakuweza kunyakuwa tuzo ya kimataifa, lakini hilo halijamkatisha tamaa kutokana na kile anachoamini kukubalika na mashabiki wake ni tuzo pekee kwake.

Wachambuzi wa muziki wanasema unapotaja wasifu wa msanii, Barnaba anashika nafasi ya kwanza kutokana na kukamilika kwa kila eneo, kuanzia uimbaji, utungaji, upigaji ala na kuburudisha.

"Kimsingi Barnaba ndiye msanii pekee Tanzania mwenye uwezo wa hali ya juu wa kuimba, kutunga na kupiga ala ya muziki. Hili linamfanya kubaki katika masikio ya watu kwa miaka yote," amesema Patrick Moses.

BASI SAWA

## Furaha Sophie atoa siri ya 'Ishara'



Mwimbaji anayekuja kwa kasi kutoka Australia, Furaha Sophie, amewashukuru mashabiki kwa mapokezi mazuri ya wimbo Ishara aliomshirikisha Christina Shusho.

Akizungumza na BT, Furaha anasema wimbo huo umebebwa na kitabu cha kutoka 12:13-14 ndio maana umekuwa na mguso wa kipekee kwa yeyote atakayeusikiliza.

"Ni wimbo wa majira haya, ni wimbo wa kutia moyo wa kuonyesha kwamba Mungu ameendelea kutumia ishara kuvusha watu kwenye hatua moja kwenda nyingine, video tayari imetoka ipo kwenye chaneli yangu ya YouTube watu wanaweza kwenda kuitazama na kubarikiwa," amesema Furaha mwenye asili ya Kongo DRC.

## Ali Kiba ulichomfanyia Barnaba inatosha



NYOTA wa Bongo Fleva, Ali Kiba amemliza mwanamuziki mwenzake Barnaba, ambaye amesema kamwe hatamsahau kutokana na kile alichomfanyia wakati akisaka nafasi ya kimuziki.

Kupitia ukurasa wake wa Instagram, Barnaba ameandika kwa kumuita ndugu yake kipenzi kutokana na msaada mkubwa wa kumpa moyo kila siku.

"Asante sana kwa upendo na nafasi kubwa ya uliyonipa, ukweli nashukuru nakumbuka uliniambia Barnaba baada ya hapa sitaki kukuona unashuka nami nimetimiza kile ulichonipa," ameandika Barnaba.



## Gigy Money kaja na hili....

MSANII wa Bongofleva na filamu, Gigy Money amesema yupo tayari kufanya kila kitu kwa ajili yake na kamwe hawezi kusikiliza ya watu.

Amesema anatamani kufanya upasuaji wa kubadilisha umbo kama akipata pesa za kutosha, licha ya kutarajia maneno mengi kutoka kwa watu mbalimbali endapo akifanya hivyo.

"Nikipata pesa naweza kufanya upasuaji, mimi sio mtu wa kuangalia maeneo mengine napenda matiti makubwa lakini naogopa athari za kiafya," amesema Gigy.

## Mke Jina: Pekua pekua, kuku kakosa mwana

**Na Adam Fungamwango**

WAKATI mwingine kuchagua sana vitu, mwishowe unapata kile ambacho hakistahili, au ambacho hukukusudia.

Pamoja na kwamba ni lazima binadamu uwe makini unapochagua kitu chochote, lakini isiwe namna ambayo unataka kujifanya kama wewe unajua zaidi kuliko Mwenyezi Mungu.

Hebu leo tuiangalie filamu inayoitwa 'Mke Jina', inayomhusu kijana mmoja aliyewaogopa na kuwakataa wanawake wa mjini na kuamua kwenda kijiji, akidhani kuwa huko ndiko atakuta wachumba ambao ni watulivu na wenye tabia njema.

Hakuutambua ule msemo usemwao mke mzuri hutoka kwa Mungu.

Imechezwa na Vaileth Issa akicheza kama Mwajuma, Abdallah Muki kama Mashaka, Said Abdallah yeye alicheza kama Baba mzee Ndole, Mariam Mohamed kama Samira, Abbas Abdallaah, Sultan Katundu, Ally Makoroboi na wengineo.

Mashaka, alikuwa akisikia stori ya vijiweni kuwa wanawake wa mjini si wa kuoa kwa sababu ni wajanja, hawashikiki na wanaonekana macho juu, na wanayajua ya mchana na ya usiku.

Stori zikamwambia kuona ni kijijini kwa sababu huko wanawake wengi wa watulivu, wana heshima na adabu, wasiojua mambo mengi ya kimjini na starehe zake.

Anatoka mjini na kwenda kijijini kusaka mwanamke wa kuoa. Baba yake mzee Ndole na dada yake Samira wanamshangaa na kumuuliza kwani mjini hakuona mwanamke yoyote anayemfaa?

Yeye akadai anataka mwanamke wa kijijini. Katika pitapita yake anakutakana na msichana mmoja anayeitwa Mwajuma. Anampenda. Analifikisha hilo kwa baba na dada yake. Wanaonekana kushangaa, lakini baba kwa utu uzima, anambariki akisema hilo ni chaguo lake, yeye hawezi kuzuia. Lakini Samira anakataa kaka yake asimuoe. Hata hivyo hana nguvu ya kuzuia. Harusi inafanyika, Mashaka na mkewe wanakwenda mjini.

Mwajuma anakutana na kinadada wa mjini, wanamchangamsha, licha ya kwamba na yeye mwenyewe yumo, hajambo kwenye mambo ya kimjinimjini, licha ya kukaa shamba.

Kila siku kiguu na njia. Kila siku vijora, vijora na yeye. Shughuli ya nani itokee impite? Hata kama mumewe hana pesa ya kijora atachukua hiyo hiyo ya kula anakwenda kununua, wanalala na njaa.

Mwajuma si wa kupika dada. Si wa kupakua. Kuna siku akaenda kwenye shughuli ya mama Mwanaheri akarudi asubuhi. Kalewa mbwiii. Akagombana na mumewe. Mashaka kavumilia. Lakini hali iliendelea kuwa mbaya.

Mke ndiyo anakuwa wa mwisho kurudi, mume akiondoka na yeye kabandua mguu, mwisho yakamfika hapa. Akaamua kumpa talaka.

Kitendo hicho kilimshtua na kumliza kwani hakutegemea, tayari alishaanza kutunzwa na kupewa kila anachohitaji na mumewe. Lakini sikio la kufa halisikii dawa. Akalia kilio cha mbwa mdomo juu, akifikiria kurudi tena kijijini na kuanza upya maisha ya bushi na kujitafutia mwenyewe.





## Kilichosababisha kifo cha Erick

IMEFAHAMIKA kwamba kifo cha mchekeshaji wa filamu Erick kilitokana na kuugua maradhi ya kifua kikuu na alikuwa akianza kupatiwa matibabu.

Rafiki wa msanii huyo ambaye alikuwa akiishi naye, amesema ugonjwa huo waligundua siku chache kabla ya kifo chake.

Amesema hali ya kuugua alianza kidogo kidogo na walikuwa wakienda hospitali kwa ajili ya matibabu.

"Erick alikuwa akiugua kifua kikuu na iligundulika siku chache baada ya kifo chake, tulikuwa tunapambana kwenda hospitali kila wakati lakini juzi alituacha," amesema Dogo Ziro.

## MIPASHO KWENYE MUZIKI WA DANSI

**Na Adam Fungamwango**

USIDHANI taarabu tu ndiyo kuna nyimbo za kupigana vijembe, mafumbo na mipasho, hata kwenye muziki wa dansi zipo.

Leo tunawaletea baadhi ya nyimbo za dansi ambazo zilikuwa na vijembe kwenda kwenye bendi nyingine au mwanamuziki waliomkusudia.

Pamoja na hayo, uzuri wa nyimbo hizo zilikuwa hazitaji mtu jina wala aliyekusudiwa, ila wenyewe pamoja na mashabiki wanakuwa wameshajua nani amelengwa.

### Radhi ya Wazazi - Juwata Jazz Band

Ulitungwa na kiongozi na mpiga solo wa bendi ya Juwata Jazz, Msondo Ngoma, Said Mabera mwanzoni mwa miaka ya '80. Dhana ya wimbo huu ni kwamba Mabera alimuimba mwanamuziki mmoja aliyehama kwenye bendi hiyo na kwenda bendi nyingine hasimu.

Inasemekana kuwa mwanamuziki huyo alikuwa anaishi kwa wakwe zake. Kwa hasira ya kuhama, Mabera alimtungia wimbo huo aliokuwa na baadhi ya maneno haya. 'Wakwe zako wamenifuata, kunilalamikia unawabana humu ndani. Kati ya wewe na mkeo nani kaolewa, wamechoka kulisha mke na mume.'

### Pole Mzee -DDC Mlimani Park

Hayati Shaaban Dede ni mmoja wa watunzi wazuri wa nyimbo na vijembe. Wakati akiwa Sikinde katikati ya miaka ya '80 alitunga wimbo uitwao 'Pole Mzee.' Ni kibao ambacho inadaiwa aliitungia bendi yake ya zamani wa Msondo Ngoma. Wachunguzi wa masuala ya muziki wanasema kuwa alikuwa akiwakejeli kuhusu wanamuziki wengi wa bendi hiyo kuhamahama na kwenda bendi zingine.

'Watoto wamekimbia nyumbani umebaki na wajukuu pia watasambaa. Iliyobaki nitamuuliza shemeji una kasoro gani hapo nyumbani. Jirekebishe na hao waliosalia wasiondoke. Pole mzee.' Ni baadhi ya maneno ya vijembe kwenye wimbo huo.

### Mv Mapenzi No 2-DDC Mlimani Park

Ni wimbo uliotungwa mara tu baadhi ya wanamuziki wa Sikinde walipohama kwenda kujiunga na Orchestra Safari Sound (OSS) na kuasisi mtindo wa Ndekule. Awali kulikuwa na wimbo wa MV Mapenzi, lakini ukatungwa namba mbili yake katikati ya miaka ya '80. Maudhui ya wimbo huu moja kwa moja ulionekana kuwalenga walioihama bendi hiyo wakiongozwa na Muhidini Maalim Gurumo.

### Chatu Mkali-OSS

Wimbo huu ni kama jibu la wimbo wa 'Mv Mapenzi'. Ulikuwa ni utunzi wa Bitchuka mwaka 1985, ambaye alikuwa mmoja wa waliohama kutoka Sikinde.

Baada ya wimbo wa Sikinde na wao walitunga kibao cha kuujibu wimbo huo, wakitoa onyo kali kwa wanaomchezea chatu. Pamoja na kwamba ni kijembe, lakini ulitungwa kwa staili ya lugha ya picha.

'Usimchezee Chatu, dongo usimtupie utaukosa ushindi. Natoa onyo kwa yoyote anayechezea chatu, atakuwa hapati lolote la manufaa na ajali imkute bila ya kutegemea, atakuja aadhirike ajute na dunia.'

### Mtoto Akililia Wembe-DDC Mlimani Par



Butchuka, akiwa OSS alitunga kibao cha 'Homa Imenizidia', dhana ya wimbo huo ni kama vile alichoshwa na maisha ya kule aliko. Lakini aliimba kama mwanamke aliyedanganywa na kumucha mumewe kwenda kuolewa na mtu mwingine, lakini asipate kile alichoahidiwa.

Sikinde, bendi ambayo alikuwa ametoka kwenda OSS, inatunga wimbo ulioonekana kama kuujibu wimbo wake. Ulitungwa na Cosmas Chidumule ambaye kwa sasa ameokoka.



# Mwigizaji Hollywood afariki

TASNIA ya filamu za Hollywood, imempoteza msanii nyota Anne Heche, ambaye amefariki dunia baada ya kupata ajali.

Mwigizaji huyo wa filamu aliaga dunia muda mfupi baada ya kukimbizwa hospitali kutokana na kupata majeraha mabaya.

"Tumepoteza nuru angavu, roho nzuri na yenye furaha zaidi, mama mwenye upendo, na rafiki mwaminifu. Anne atakumbukwa sana lakini anaendelea kuishi kupitia wanawe na kazi yake ya ajabu," mwakilishi wa Heche aliambia Page Six.



## Armstrong akana ubakaji

MWIGIZAJI mkongwe kutoka Nollywood Moses Armstrong, amekana kuhusika na kitendo cha ubakaji na kueleza Mungu pekee anajua.

Msanii huyo wa filamu za Kinigeria, kupitia ukurasa wake wa Facebook, amesema kamwe hajabaka msichana mdogo kama anavyoaminika na wengi.

"Hakuna kitu kinachompita Mungu. Ukiamini utapokea. Sikumbaka mtu yeyote. Sijawahi kubaka na sitabaka kamwe. Nimerudi kwa nguvu zaidi, nina furaha niliienda gerezani, Mungu aliienda pamoja nami," aliandika.

Armstrong alikamatwa na polisi wa jimbo la Akwa Ibom mwezi Juni kwa madai ya kumnajisi msichana wa miaka 16.

## ASAP bado limemganda

RAPA wa Marekani ASAP Rocky, anakabiliwa na mashtaka ya kufanya shambulio kwa kutumia silaha.

ASAP anatuhumiwa kushambulia kwa kufyatua risasi mwaka jana huko Los Anjeles.

Rapa huyo anachunguzwa na LAPD kwa madai ya kuhusika katika ufyatuaji risasi Novemba 6, mwaka jana.





## 2Face kweli kuna mama kijacho?

Mwanamuziki wa Nigeria Innocent Idibia, maarufu kama 2Face, amejitokeza hadharani na kuwakejeli wale wote wanaodai amempa ujauzito mfanyakazi wa benki.

Nyota huyo wa muziki aliandika kupitia ukurasa wake wa Instagram, akisema uvumi huo unaoenezwa na watu waliochanganyikiwa ubongo.

" Ukiona watu ambao hawajui hata ni jina la seneta wao huwezi kuwaambia ukweli wanadhani wanatukanwa, Baba wasamehe kwa sababu ubongo wao umechanganyika," aliandika.

## Buju majigambo yamekuponza

MWANAMUZIKI nyota wa Nigeria Buju BNXN, amebanwa na jeshi la polisi baada ya kujigamba hadharani kuwa alimtemea mate ofisa wa jeshi hilo.

Msemaji wa Kamandi ya Polisi ya Jimbo la Lagos, Benjamin Hundeyin kupitia ukurasa wake wa Twitter kwamba lazima atawajibika kwa kitendo hicho.

BNXN aliandika kwenye Twitter kwamba alimtemea mate ofisa wa polisi usoni na alijisikia vizuri.

Tangu wakati huo msanii huyo ameifuta tweet hiyo.



MAKALA

# Uwekezaji wa pamoja husaidia kutimiza malengo ya wengi

**Na Mwandishi Wetu**



Viongozi wa Mfuko wa Uwekezaji wa UTT-AMIS.

KUNA mbinu tofauti ambazo watu hutumia kuwekeza katika miradi mbalimbali kwa malengo ya kunufaika kiuchumi.

Uwekezaji huo unaweza kufanyika katika kilimo, misitu, madini, uvuvi, masoko ya fedha na mitaji. Lengo kuu ni kujiongezea kipato na kumudu gharama za maisha kwa mtu mmoja mmoja, makundi na taifa kwa ujumla.

Hata hivyo, wawekezaji na kampuni kubwa, wanaweza wakachangisha pesa kutoka kwa wadau mbalimbali katika jamii kwa ajili ya kufanya biashara, kampeni dhidi ya jambo fulani, au miradi.

Jambo muhimu linalopaswa kueleweka ni kwamba, mtaji wowote chanzo chake kinatoka kwenye jamii husika na hata benki ambazo hujiendesha kwa kutoa mikopo tegemeo kubwa ni wanajamii.

Mkurugenzi wa Masoko, UTT AMIS, Daud Mbaga, anafafanua kuhusu uwekezaji huo kwamba siku hizi si jambo geni watu wakijiinua kwa kupitia vikundi vya vikoba na jumuiya za uwekezaji.

Vikundi vya aina hiyo, vyote vina nia moja, nayo ni kuweka na kuwekeza fedha kwa ajili ya kuboresha maisha.

"Wakati mwingine jamii hukusanya pesa zisaidie mambo ya heri au hata majanga yanapotokea cha muhimu hapa ni nguvu ya umoja," anasema Mbaga na kuongeza "Kwa dhana hii watu mbalimbali, kampuni, taasisi zinakusanya fedha pamoja kwa lengo fulani. Wakusanyaji wanakuwa watu tofauti wenye elimu na uzoefu wa jambo ambalo ni muhimu kwenye kutimiza lengo la kukusanya pesa hizo, iwe msaada kwa wengine, uwekezaji au ujenzi katika jamii."

Anasema, pamoja na malengo ya kila uwekezaji kunatarajiwa kuwa mema, zipo changamoto za kukusanya fedha kwa kuwa vichwa vingi ni ngumu kuvifanya viwe na mtazamo mmoja.

Anaeleza, wanaochangia kwenye kapu moja ni lazima kuwa na lengo ambalo ni bayana lenye uwazi kwa kila mtu na lengo liwe na faida au matarajio mazuri kwa jamii.

"Mfano uwekezaji wa pamoja kupitia mifuko ya UTT AMIS. Lengo lake ni kukusanya fedha na kuziwekeza ili kuwapa wawekezaji wa fedha hizo faida shindani. Lengo laweza kuwa faida ambayo mwekezaji anaipata kama gawio au kama faida kwenye biashara nyingine yoyote ile," anasema.

Mbaga anasisitiza kwamba, faida za jamii kuungana na kufanya uwekezaji kwa ajili ya lengo fulani ni nyingi, ikiwamo kupunguza gharama za uwekezaji.

Kwa mfano, ili kuwa na biashara ya mtaji wa milioni 10, watu wawili walioungana na kila mtu atatao shilingi milioni tano, ingawa wakiwa watu wanne kiasi kitapungua na kila mtu atatoa shilingi milioni 2.5.

"Mradi unaohitaji pesa nyingi, ni vigumu kwa mtu wa kawaida kumudu gharama zake. Kwa mfano ili kununua hati fungani mwekezaji anapaswa kuwa na walau shilingi milioni moja, pia akaunti za muda maalumu ni kuanzia shilingi laki tano, milioni moja," anazidi kueleza.

"Laki tano kama mtaji ni hela ndogo lakini bado ni nyingi kwa mwananchi wa kipato cha chini kwenye uwekezaji wa pamoja mtaji ni kuanzia shilingi elfu kumi, na watu wakichanga pamoja pesa zinakuwa nyingi," anazidi kufafanua.

Kwa maelezo ya Mbaga, ni kwamba pesa zikiwa nyingi kwa pamoja zinaweza wekeza na kufikia mabilioni iwe kwenye akaunti za muda maalumu, hati fungani, majengo, vyombo vya usafiri na sehemu nyingine nyingi.

Anaongeza kwamba, uwekezaji wa pamoja, kila mmoja ni balozi. Kampuni kubwa zenye wawekezaji wengi pia zinajikuta wenyewe wakiwavutia wawekezaji wengine kwa njia ya mazungumzo kupitia madaraja mbalimbali.

"Hii inapunguza gharama za kutafuta masoko, wawekezaji pamoja hutumia njia mbalimbali licha ya mazungumzo ya uso kwa uso, njia hizo ni kama vile simu, tovuti, mitandao ya kijamii kama Facebook, Instagram, Twitter," anasema Mbaga.

**KULINDA MTAJI**

Mbaga anasema kwamba, wachangiaji wakiwa wengi, lazima kuwe na daraja litakalokutanisha wenye kutoa na wenye kupokea pesa, hivyo muhimu kuwapo kwa tamko lililo wazi la kuwataka watu washiriki kwenye uwekezaji kwa makubaliano maalumu ili kupata manufaa fulani na zaidi ikiwa faida.

"Uwekezaji wa pamoja kwenye mifuko ya uwekezaji huwa wanaweka masharti husika kwa madhumuni ya kupata faida. Kwenye uwekezaji wa pamoja, wenye pesa watatoa kwa meneja awekeze kwenye sehemu walizokubaliana, kwenye baadhi ya kampuni zilizoorodheshwa kwenye Soko la Hisa la Dar es Salaam, au kampuni binafsi yenye uhitaji," anabainisha.

Pia wanaweza kukopesha benki kupitia akaunti za muda maalumu na kuikopesha serikali kupitia hati fungani za muda mfupi au za muda mrefu.

Mifuko ya uwekezaji wa pamoja kama mfuko wa Ukwasi, na Hati Fungani yote inayosimamiwa na UTT AMIS, ni mifuko ambayo imekuwa ikitoa faida, hukusanya pesa kwa madhumuni ya kuzikopesha kwenye sehemu zilizotathminiwa kwa uhakika wa kiasi kikubwa kuwa faida itapatikana.

"Hisa zinalipa hasa pale mwekezaji anapokuwa hana haraka, ili kuzipa nafasi ya kukabiliana na changamoto za kupanda na kushuka kwa thamani kwa kampuni fulani au kwa soko lote la hisa. Kimsingi uwekezaji kwenye hisa kama uwekezaji kwenye sehemu nyingine unahitaji utaalamu na wakati mwingine uvumilivu ni muhimu," anasisitiza.



Uwekezaji wa pamoja unaweza kuwa katika migodi mikubwa ya madini.

TULIKOTOKA, TULIPO & TUNAPOKWENDA...



Na Adam Fungamwango

# Kutoka picha za kusafisha studio hadi 'selfie'

## ■Mpigapicha mzuri lazima awe na mikogo
## ■Ndiye anayepanga pozi, nani akae wapi

TUNAONA siku hizi ambapo teknolojia imekuwa sana duniani kupiga picha imekuwa si stori kubwa kama zamani.

Siku hizi picha unajipiga mwenyewe. Wanaita 'selfie'. Unaweza kumpa mtu akakupiga kwa kutumia kamera za kisasa ambazo zinakuwa na mwonekano mzuri sana. Wakati mwingine mtu anajipiga mwenyewe kwa kutumia simu za mkononi, maarufu kama simu janja au 'smartphone.'

Vyovyote vile ukipenda, unaweza kumpa mtu simu hiyo akakupiga unavyotaka.

**KARIBUNI TULE**

Tunaona kwenye mitandao ya kijamii watu wanavyopigwa au kujipiga picha na kuzituma.

Kuna wanaopiga picha wanaendesha magari, wapo wanaotembea kwa miguu, achilia mbali kwenye matukio mbalimbali ya kijamii. Kutokana na urahisi wa kupata picha popote pale mtu alipo kutokana na simu za mkononi za kisasa kuwa na uwezo wa kuchukua picha, imekuwa kama fasheni hivi sasa.

Kuna wataopiga kwa ajili ya kuonyesha nyumba zao, magari na mali zingine. Hata kama wakati mwingine si nyumba wala magari yao, bali ni ya kuazima, anaweza akasema yake. Kumekuwa na maisha yasiyo ya uhalisia kwa watu wengi wa sasa, kwani anaweza kwenda kwa rafiki yake anapiga picha akaiposti akisema ni ya kwake.

Kuna wanaoposti picha kuonyesha urembo wao. Kwenye simu hizi sa kisasa pia kuna sehemu ambazo yoyote anaweza kuirekebisha na kuiremba picha yake na kuonekana mzuri au mrembo zaidi kuliko alivyo kiuhalisia. Huwezi kuona hata chunusi.

Wapo wanaopiga picha wakiwa ofisini, na hata wakati wa kula, atapiga chakula na kukiposti na kuwaambia wanaomfuata kwenye mtandao wake wa kijamii 'karibuni tule.'

**WAPIGWA PICHA ZAMANI**

Haya yote tunayoyaona hawakuwapo zamani. Wanaoishi katika zama zote mbili wanakubali kama ni maendeleo makubwa yamepigwa duniani hadi leo hii hasa kwenye masuala ya teknolojia.

Kwanza kabisa kabla ya kuwepo kwa teknolojia ya wapigapicha wa mitaani, watu walilazimika kwenda studio.

Na siku ya kwenda huko kama familia ni lazima mama waogoshe watoto wake, anawalishe nguo mpya au zile za kuendea safari, atawapaka mafuta na manukato ili tu waende studio wakapige picha.

Na iikifika sikukuu familia nyingi ilikuwa ni lazima waende studio kupiga picha. Huko utakita kuna madhari yaliyotengenezwa, kama vile maua ya kushika, bengi la kukaa watu kama wapo wengi, kuchora ukutani kama mbuga za wanyama, au mito na bahari, pamoja na vitu vingine mbalimbali ambavyo vitamridhisha mpigwaji ili aone ni kweli ametoa pesa yake kihalali.

Baadaye teknolojia ilivyozidi kukua, ndipo walipoanza wapigapicha wa mitaani.

Hao walikuwa wakizunguka mitaani, kwenye sherehe za kijamii au zingine zinazofanana na hizo kwa ajili ya kupiga picha.



Wanamuziki wa bendi ya Afro 70, wakiwa na kiongozi wao Patrick Balisidya (aliyesimama kulia), wakiwa kwenye pozi ya picha iliyopigwa miaka ya 1970, na hiyo ilikuwa ndiyo staili ya ukaaji wa picha za zamani au zinazofanana na hivyo, zilizopigwa na kameramani na kwenda kusafishwa studio.



Mrembo akijipiga picha mwenyewe na simu ya mkononi maarufu kama 'selfie' na kuonyesha jinsi binadamu walivyotoka kwenye telnolojia ya kupigwa picha na kusubiri mwezi mzima, hadi kujipiga mwenyewe ikionekana hapo hapo.

Na baada ya kupiga inachukua muda wa kuanzia wiki moja na kuendelea hadi kurudi tena kuzileta picha hizo baada ya kumaliza kuzisafisha. Inawezekana ikakaa hadi mwezi kwa sababu anapiga picha na hadi mkanda umalizike ndiyo aende studio kuzisafisha.

Wadau mbalimbali mada hii ilipowekwa kwenye mtandao wa kijamii wamefunguka kuhusu walivyokuwa wakipigwa picha na 'makameramani' wa wakati huo.

"Hahahaaa mkuu umenikumbusha mbali sana...ziliwahi kuungua picha za tukio moja muhimu sana.

Tumetoka mbali. Zamani ili uonekane mjanja na umeendelea ilikuwa lazima upige picha, na zilikuwa 'black and white.' Kweli kila kitu na wakati wake.

Mmoja aliuliza ni kitu gani kilikuwa ninasababisha picha kuungua wakati huo? Ndipo mwingine akamjibu.

"Picha zilikua 'zinaungua' kwa makosa ya mpiga picha au studio ya kusafisha picha.

Mpigapicha akikosea kutoa 'film', na ikipata mwanga tu kwisha kazi.

Hivyo hivyo studio nao wakikosea kuitoa, na ikaingia mwanga, inaungua.

Unaweza kupoteza picha za matukio ambayo hayawezi kurudiwa harusi au matukio ya kijamii.

Aisee nimekumbuka mbali sana." Mdau mwingine alijibu.

"Kumaliza darasa la saba miaka ya 1980, tulilipia darasa zima pesa, tukapicha picha, halafu mwisho wa siku zikaungua zote Tulisikitika sana." Mchangiaji mwingine alileta mchago wake.

Mdau mwingine yeye alieleza kuwa bila kuwaka 'flash' yeye anaona kama hajapigwa picha.

"Hakuna tukio lilinikera wakati huo kama kupigwa picha bila flash, nilihisi sijapigwa picha."

Ni kweli kuna wakati wapigapicha wengine walikuwa hawawashi mwanga, na hiyo ilitegemea sehemu yenyewe kama ina mwanga au giza. Kama ina giza, 'flash' inahitajika.

Lakini wapigapicha walikuwa wanatumia 'flash' kuwapoza watoto waliokuwa wanalilia kupiga picha.

Anawapanga na kuwawashia 'flash' picha kupiga picha, ikiwaka, watoto wote wanadhani tayari wameshapigwa.

Hata hivyo wengine walitumia hilo kufanya udanganyifu kama mdau huyu anavyosema.

"Nakumbuka mwishoni wa miaka ya tisini, Songea mjini pale alikuwa mpigapicha mmoja alipiga watu 'flash' mtaani akachukua pesa na kuondoka kabisa mjini hapo, hakuonekana tena."

**MBWEMBWE ZA WAPIGAPICHA**

Wapigapicha au makameramani wa zamani walikuwa na mikogo au mbwembwe zinazofanana.

Kwanza kabisa kamera yake ni lazima iwe na kamba nyeusi kaining'iniza shingoni.

Halafu asilimia kubwa walikuwa na baiskeli kwa sababu ya kumrahisishia kazi ya kuzungukia wateja, nyuma ana begi ambalo lina picha za watu ambao hawajamaliza madeni ili awakabidhi.

Anakupiga picha na anakwambia picha yako utaipata panapo majaliwa mkanda ukijaa. Sasa hapo ni kunzia wiki moja kwenda juu wakati mwingine hadi miezi miwili.

Huyo ndiye anatewapangia anayempangia anayepigwa pozi gani akae ili picha itoke vizuri.

Hata picha ya familia, anaweza yeye ndiye akawapanga wote, hadi baba akae vipi na afanya nini ili kumpa urahisi wa yeye kupiga vizuri.

Kwa sababu ya umuhimu wao wakati huo, wengi wao walikuwa ni watu wa majivuno sana.

Anaweza kupita mtaani akaitwa, lakini huyo... na baiskeli yake, hasimami.

Wakati sikukuu inakaribia, watu wanaweka oda kwa mpichapicha wiki mbili kabla na akija kwanza anaanza kula pilau na soda yake ambavyo vinakuwa vimehifadhiwa kwa ajili yake tu, baada ya hapo ndiyo anapiga picha.

Yeye ndiye anayetafute eneo siku hizi wanaita 'lokesheni', kama kwenye maua, majani, gari au sehemu yoyote anayoona inafaa na anaelekeza hadi mapozi.

Mdau mmoja akapigilia msumari akidai kuwa kama kameramani hata mbwembwe au mikogo watu hawampendi kwa sababu anaonekana si mpigapicha mzuri

"Kwanza mtu wa kamera enzi hizo kama hana mbwembwe wala madoido huyo hamumwiti tena ilikuwa mnaona ile mikogo ndiyo picha itatoka vizuri, yaani anakwambia haya napiga sasa, mara aaah wewe sogea ndani kidogo, mara na wewe kwanini umeinama sasa? Yaani mpaka apige mko hoi.

**0716 350534**

HABARI KIMATAIFA

# Marekani yataka kukabidhi madaraka kwa njia ya amani

**NAIROBI, Kenya**

SENETA wa Marekani, Chris Coons anayeongoza ujumbe wa wabunge wanaofanya ziara nchini Kenya, amesema kuwa amemuhimiza rais anayeondoka madarakani, Uhuru Kenyatta kuhakikisha anakabidhi madaraka kwa njia ya amani.

Kauli hiyo aliitoa baada ya kumaliza mikutano yake na Rais Kenyatta, pamoja na wagombea wawili wakuu wa urais, Raila Odinga na William Ruto. Coons aliliambia shirika la habari la AP kwamba alitiwa moyo katika mikutano yote mitatu kwa kusikia misimamo ya wito wa utulivu na kuheshimu michakato ya kisheria iliyoko katika katiba ya mwaka 2010.

Coons aliongeza kuwa mazungumzo hayo yalihusu utawala wa kisheria, umuhimu wa uchaguzi huru na haki na kukabidhi madaraka kwa amani.

Seneta Coons aliweka wazi kuwa Marekani inapaswa kujifunza kwa Kenya kutokana na kupitia wakati mgumu katika masuala ya uchaguzi katika muda wa miaka michache iliyopita akimaanisha shambulizi la Januari 6, mwaka 2021, dhidi ya jengo la bunge la nchi hiyo wakati aliyekuwa Rais Donald Trump alijaribu kubaki madarakani.

Coons alimpongeza rais huyo kwa kuheshimu katiba na kuondoka madarakani baada ya mihula miwili.

Aliongeza kuwa walizungumzia baadhi ya majukumu muhimu ambayo ametekeleza kikanda kusaidia katika mazungumzo nchini DRC, Ethiopia na kumhimiza Rais Kenyatta kufikiria kuhusu njia baada ya urais wake kukamilika ambapo anaweza kuendelea kuchukua jukumu la kujenga amani ya kikanda.

Coons alisema hakwenda Kenya kutafuta kitu kama makubaliano ya kushiriki katika uongozi wa pamoja ambayo Kenyatta na Odinga walikuwa nayo na kumaliza miezi ya mivutano baada ya uchaguzi mkuu wa mwaka 2017 ambao matokeo yake yalibatilishwa na mahakama ya juu kutokana na kasoro za uchaguzi.

Taarifa kutoka ofisi ya rais, ilisema kuwa Kenyatta amemwambia Coons kwamba Kenya itadumisha nafasi yake ya kuwa mfano wa kuigwa wa demokrasia barani Afrika kwa kudumisha amani wakati wa kipindi hicho cha kukabidhi madaraka.

Kenyatta alikuwa amemuunga mkono Raila Odinga katika uchaguzi wa Agosti 9 baada ya kukosana na naibu wake William Ruto ambaye alishinda kinyang'anyiro hicho cha urais kwa kura chache.

Kiongozi huyo anayeondoka madarakani bado hajampongeza hadharani Ruto, ambaye amehudumu kama naibu rais tangu 2013 na kwa muda mrefu alikuwa akichukuliwa kama mrithi wa Rais Kenyatta.

**DW**



Watu wakiangalia roboti iliyoundwa katika umbo la samaki katika maonyesho ya teknolojia ya roboti duniani yaliyofanyika Beijing, China juzi. **PICHA: AFP**

# Miili 20 iliyokaushwa yagunduliwa

**ABUJA, Nigeria**

JESHI la polisi kusini mwa Nigeria, wamewakamata watu watatu kuhusishwa na tukio la kugunduliwa kwa miili ya watu 20 iliyokaushwa karibu na mji wa Benin katika jimbo la Edo.

Miili hiyo ilipatikana katika jengo linaloshukiwa kutumiwa kama kaburi la voodoo.

Msemaji wa polisi, Chidi Nwabuzor, ameiambia BBC kwamba maiti hizo ni 15 za wanaume, wanawake watatu na watoto wawili.

Haijawa wazi ni kwa muda gani zimekuwa eneo hilo.

Aliongeza kuwa maofisa wa polisi wenye silaha na walinzi wa eneo walikuwa wamevamia jengo hilo lililopo nje ya mji kufuatia taarifa waliyopewa kwa siri.

Ugunduzi wa miili hiyo umewashtua watu nchini Nigeria na wakazi wa eneo hilo ambao walisema wametishwa na tukio hilo.

Wengi wanauliza ni kwa vipi miili hiyo iliweza kufichwa pale bila majirani kufahamu.

**BBC**

# Kinu kikubwa cha nyuklia chaleta hofu duniani

**LVIV, Ukraine**

KATIBU Mkuu wa Umoja wa Mataifa, Antonio Guterres na marais wa Uturuki na Ukraine wamejadili njia za kuvimaliza vita vilivyoanzishwa na Russia nchini Ukraine.

Viongozi hao wanataka vita hiyo kufikia kikomo ili kukilinda kinu kikubwa zaidi cha nishati ya nyuklia barani Ulaya.

Wakati mkutano ho unafanyika, Russia na Ukraine zinalaumiana kuhusiana na mashambulizi yaliyofanywa karibu na kinu hicho.

Guterres aliwaambia waandishi wa habari baada ya mazungumzo mjini Lviv kwamba ana wasiwasi kuhusiana na yanayoendelea katika kinu cha nyuklia cha Zaporizhzhia.

Guterres ametaka wanajeshi na silaha kuondolewa nchini humo.

"Ni lazima akili itumike ili kusiwepo na vitendo vitakavyohatarisha usalama wa kiwanda hicho cha nyuklia. Kinu hicho hakistahili kutumika kama sehemu ya operesheni yoyote ya kijeshi badala yake, kunahitajika makubaliano ya dharura ili kuhakikisha kwamba Zaporizhzhia ni muundo msingi wa kiraia na kuhakikisha usalama wake," alisema.

Rais wa Uturuki, Reccep Tayyip Erdogan na Volodmyr Zelensky wa Ukraine, walisema watatumia hali nzuri iliyoko sasa ili kufufua mazungumzo ya amani na Russia yaliyofanyika Istanbul mnamo mwezi Machi

Katika hatua nyingine, Rais wa Uturuki Tayyip Erdogan amesema atazungumza na Rais wa Russia, Vladimir Putin kuhusu suala la kinu cha nyuklia cha Zaporizhzhia baada ya kufanya mazungumzo yake na Zelensky. Zelensky aliomba Russia iondoe shughuli zake zote karibu na kiwanda hicho wakati wa mkutano huo, Erdogan aliwaambia waandishi wa habari akiwa kwenye ndege yake akirejea Uturuki.

"Tutajadili suala hili na Putin na kumuomba haswa Russia kufanya kile inachopaswa kama hatua muhimu kwa amani ya ulimwengu," alisema.

Ziara ya Erdogan nchini Ukraine ilikuwa ya kwanza tangu Russia ilipovamia nchi hiyo mapema mwaka huu.

Russia kupitia kwa Naibu Waziri wa Mambo ya Nje, Sergei Ryabkov, aliyenukuliwa na shirika la habari la Reuters, alisema wanajeshi wanaodhibiti kinu hicho wanalenga kuzuia maafa yaliyotokea Chernobyl mwaka 1986 yasitokee tena.

Tukio hilo lilichukuliwa kuwa ajali mbaya zaidi ya nyuklia duniani.

**DW**

TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

Ndugu **FUMBUKA NKWABI NG'WANAKILALA** amepoteza kadi ya gari namba **T949 DBV** aina ya **Nissan Navara**.Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi. Taarifa ya kupotea kwa kadi imetolewa katika kituo cha Polisi. RB namba **DAR/OST/RB/330202/2021**

## KUPOTEA KWA VYETI



**MUDA L MGWILANGA** anatangaza kupotea kwa vyeti vya taaluma: cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S2226-0019** kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia **MASISIWE SECONDARY SCHOOL** mwaka **2009,** cheti cha ualimu ngazi ya **CERTIFICATE** chenye usajili namba **E0603-0045** kilichotolewa na **MUFINDI TEACHERS' COLLEGE** mwaka **2014,** cheti cha **DIPLOMA IN PRIMARY TEACHER EDUCATION (DPTE) na TRANSCRIPT OF EXAMINATIONS RESULTS** zenye usajili namba **ND2016986785 VILIVYOTOLEWA NA OPEN UNIVERSITY OF TANZANIA mwaka 2018.** Kwa yeyote atakaeviona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

**POLISI TAARIFA: TAB/RB/3805/2021**

## KUPOTEA KWA CHETI



**JOSEPHINE YAMBI** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba **P0332-0046 CSEE** kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia **MOROGORO SECONDARY SCHOOL** mwaka 1976. Kwa yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

**POLISI TAARIFA: KW/RB/3924/2022**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**YUDATADE ROMAN MBOWE** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya **IST** yenye namba ya usajili **T792 DRN**, Chasis namba; **NCP600093608**, Engine namba **2NZFE93608**. Kwa yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi kilichopo karibu.

**POLISI TAARIFA: DAR/URA/RB/328328/202**

## KUPOTEA KWA CHETI



**ARON JOSEPHAT KIGANDA** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S.2211.0054** kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia **MWILAMVYA SECONDARY SCHOOL** mwaka **2016.** Kwa yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

**POLISI TAARIFA: DAR/STA/RB/324852/2022**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**JACKSON KALELO BERERE** ANATANGAZA KUPOTEA KWA KADI YA GARI YENYE NAMBA ZA USAJILI **T951 AEN.** CHASSIS NO **TXD501686973** ENGINE **NO 393542 .** KWA YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI **ARU/ARU/RB/330051/2022**

## TANGAZO LA KUPOTEA KADI YA PIKIPIKI

**ALLY ISSA MSIMULIA** ANATANGAZA kupotelewa na kadi ya PIKPIKI yenye namba za usajili **MC798 AAV** Chasis Namba: **LBRSPJB5XE9012769** Engine Namba: **14924461** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi taarifa ya polisi RB namba **MKB/RB/145/2022.**

## KUPOTEA KWA CHETI



**ELIAS MARWA CHACHA** Anatangaza kupotelewa na cheti cha kuhitimu Kidato cha Nne index **No 30718-0064 Mwaka 2013** Shule ya Sekondari **NYANSINCHA,** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa **(NECTA).** Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

**Taarifa polisi: DOD/DOD/RB/294332/2022.**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**WILLIAM ANAEL MBISE** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA GARI YENYE NAMBA ZA USAJILI **T.386 DTJ**. YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI KILICHO KARIBU.TAARIFA YA POLISI **MBE/MBE/RB/329451/2022**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**BATHOLOMEW PAUL MIYANGA** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye jina **EVANGELICAL LUTHERAN CHURCH IN TANZANIA DODOMA DIOC** aina ya Toyota **LANDCRUISER PRADO** namba za usajili **T 862 DRF**. Chassis no. **JTEBH9FJ00K214167,** Engine **No.1KD2852983.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **DOD/DOD/RB/328212/2022**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**MARCO INEGEJA SILABI** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya **SUZUKI CARRY** yenye usajili namba T988 **DXP , CHASSIS NAMBA: DA63T797793** na **ENGINE NAMBA: K6A9059203**. kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

**POLISI TAARIFA: DAR/ STA/RB/ 329401/2022**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**KATIKA MAHAKAMA YA MWANZO**
**WILAYA YA MJINI MOROGORO**
**KITUO CHA MJINI**
**MKOA WA MOROGORO**

**Usimamizi wa Mirathi Na......54/2022**
**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA**
**MAREHEMU: ALLY JUMA DIFUNGILE WA MJI MPYA**
**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA USIMAMIZI WA MIRATHI**
**YALIYOLETWA NA: JUMANNE SELEMAN MBONAKUCHA**

### TANGAZO

**(kanuni ya 5(2)ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu,wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tahehe **01 Mwezi 09 Mwaka 2022** kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

**Zingatia;**

- Wosia wa marehemu huyo upo mahakaman na waweza kukaguliwa
- Marehemu hakuacha wosia wowote.

**Imetolewa leo tarehe 18 mwezi 08 mwaka 2022**

HAKIMU
MAHAKAMA YA MWANZO Mjini
MOROGORO

**HAKIMU MFAWIDHI**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**CALVIN CARLOS LEOPOLD** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya **TOYOTA 4RUNNER** yenye usjili namba **T556 AEF , CHASSIS NAMBA: JJ3HN66ROT0006978,** ENGINE NAMBA: **TTY342JGFFK.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

**POLISI TAARIFA: ARU/ARU/RB/329771/2022**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**SIMON OTHINIEL AHIA** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya **GRAND VITARA** yenye usjili namba **T490 CCZ , CHASSIS NAMBA: JSAFT152V00211138, ENGINE NAMBA: J20A222535.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

**POLISI TAARIFA: ARU/ARU/RB/329276/2022**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**MIKE NAFTAL TENGA** ANATANGAZA KUPOTEA KWA KADI YA GARI YENYE NAMBA ZA USAJILI **T567 APJ,CHASSIS** NAMBA **SX906501467** ENGINE NAMBA **1S108069.** KWA YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA POLISI. **ARU/ARU/RB/180236/2022**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI**
**IDARA YA UHAMIAJI**

| | |
|---|---|
| Telegramu: UHAMIAJI KINONDONI | OFISI YA UHAMIAJI ( W) |
| TELEFAX: +255222850595 +255222850584 | S.L.P 3315 , Dar Es salaam |
| SIMU +255222170096 | Tarehe: 18/08/2022 |
| Kumb. Na.CA.69/120/01 F31 | |

**MHARIRI WA GAZETI LA KISWAHLI**
**YAH: OMBI LA URAIA**



**MR MARINUS FORTUNE CHRISTIAN DOM** mwenye picha hapo juu, anaomba uraia wa Tanzania kwa Mh. Waziri wa mambo ya ndani ya nchi, utaifa wake wa sasa ni **ZIMBABWE** Nchiatokayo **ZIMBABWE** shughuli zake **MFANYABIASHARA** anwani ya mwajiri/biashara **S.L.P 42814 DSM** yupo hapa nchini tangu 2001 pamoja na kuishi DSM pia amewahi kuishi DSM

Kwa yeyote mwenye taarifa/sababu za kwanini mwombaji asipewe uraia wa Tanzania, atume taarifa ya maandishi kwa kamishna jenerali wa uhamiaji S.L.P 512, Dar es salaam,

**Kumb. Na. DN AC/27.340/1859**

**OFISI ZA MATANGAZO MIKOCHENI INDUSTRIAL AREA, PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.**

**MOB: +255 - 0782253676**

**TAHADHARI:** Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji **THE GUARDIAN LIMITED** hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuzi wa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# HADITHI

MGENI wa ajabu anatokea kwenye kijiji cha Semwanza, Lugoba mkoani Pwani. Anakotoka hakujulikani. Watu wote wanamwogopa. Ni kwa sababu hawamjui. Msichana Siwatu anajitolea kumsaidia mgeni huyo. Kwa kufanya hivyo, anabezwa kwa maneno mengi ya kejeli kwa kumsaidia mtu asiyemjua ambaye anaweza kuwa hatari kwa kijiji. Baadhi ya viongozi wa kijiji waliungana na wanakijiji kutaka wamtimue mgeni huyo asiyejulikana, lakini akakataa katakata. Pamoja na kutishwa kuwa atatengwa na kijiji, bado msichana huyo alisimama na msimamo wake ule ule wa kumsaidia kwa sababu alikuwa na shida kubwa. Matokeo ya haya, yanamuingiza Siwatu kwenye msukosuko mkubwa ambao hajawahi kuupata kwenye maisha yake kiasi cha kumkatisha tamaa. Fuatilia kisa hiki.

# KAMA IPO, IPO TU-19

**Na Adam Fungamwangwo**
**(0716 350534)**

"Mimi pia nawasilisha ombi langu la kutaka kukuoa."

"Kunioa?" Akauliza kwa mshangao.

"Ndiyo." Bakari akajibu kwa msisitizo.

Siwatu alichoka. Kichwa kikaanza kumuua. Mtu aliyeishi naye, akalala naye chini ya paa moja kwa miezi mitatu, hajawahi kumtamkia neno lolote la kumhitaji. Alilala chini na yeye kitandani. Licha ya wanakijiji wengi kutokubaliana na hilo, na kujua kabisa kuwa ni mtu na mpenzi wake licha ya wenyewe kukanusha, leo hii anamtamkia kuwa anataka kumuoa.

Walikuwa wanapendana sana na bado wanapendana, lakini hawakuwahi kuambiana neno lolote la mapenzi hadi Bakari anaondoka, licha ya kwamba miili na macho yao yalionekana kuhitajiana.


Siwatu, alionekana kutomshangaa Bakari kumpenda, lakini alichoshangaa na kushtuka kuwa maneno yale yamechelewa sana. Angeambiwa tangu kipindi kile ambacho anaishi kijijini pale wala asingepinga.

Na mpaka sasa bado Siwatu anampenda sana Bakari licha ya kwamba hawaambiani. Lakini tayari ameshakubali kuolewa na mwanaume mwingine.

"Bakari, mbona unanitia kwenye majaribu? Mbona unanipa majanga? Kwa nini hukuniambia mapema kabla hujaondoka? Mimi nimekataa wanaume wengi tu, nisingeshindwa kumkataa huyu ambaye simtambui. Ningekusubiri hata miaka miwili. Ni kweli Bakari mimi nakupenda sana, lakini nimeshakubali kuolewa na mtu mwingine. Hapa unanipa majaribu upya, furaha yangu yote imepotea." Akalalamika mtoto wa watu.

"Ni kweli Siwatu sikukwambia siku zote zile kwa sababu nyingi tu. Kwanza wewe ndiye ulikuwa mkombozi wangu uliyenitoa kwenye shimo la umauti. Ndiyo maana sikuweza kutamka neno hilo kwa sababu nilitokea kukuheshimu. Baadaye tulivyozoeana nikatokea kukupenda sana, lakini heshima ya mwanzo ikazidi ile ya pili ya kukupenda."

"Yaani mimi sijui hata nifanye nini. Kumkatalia jamaa nashindwa kwa sababu nimeshakubali. Ila mimi nilijua unanipenda tangu wakati ule. Na kilichonifanya nikubali ni kuona kimya kwako kimekuwa kingi, nikajua hutorudi. Lakini pamoja na kwamba hukuwahi kuniambia, vitendo vilizungumza zaidi kuwa unanipenda kuliko maneno." Akafunguka mtoto wa watu.




**"Hapana mpenzi." Bakari akasogea na kumshika Siwatu. Kwa mara ya kwanza akamshika kama mpenzi wake halisi.**

"Unajua Siwatu, hata mimi nilijua unanipenda, na ndiyo maana hata walipokuwa wanakijiji wanatuambia mimi na wewe kwa sababu tunalala chumba kimoja ni mtu na mpenzi wake wakati si kweli, kuna siku uliwajibu kwani cha ajabu nini?"

"Mhh, sasa hili tunalifanyaje mwenzangu, maana mimi hapa nimeshachanganyikiwa." Siwatu alimwambia Bakari huku akitikisa kichwa.

"Tuache muda utaongea, kama ni mimi au huyo jamaa." Ni jibu ambalo halikumridhisha Siwatu. Hapo nakuna muda wa kuongea, ila kuna utata. Siwatu alimpenda mno Bakari na alimpenda awe mama wa watoto wake. Lakini kama ilivyo kwa mila za Kiafrika mwanamke asingeweza kuanza kumtamkia mwanaume kuwa anampenda au amuoe. Lakini sasa amemwambia ukweli. Na ndicho alichokuwa akikitaka tangu mwanzo. Tatizo lilikuwa moja tu. Ameshamkubalia mtu mwingine.

**********************************

"Samahani tumekuja kutoa taarifa kuwa yule aliyetaraji kujitambulisha amepata udhuru, kwa hiyo wiki hii hatukuweza kuja naye, mpaka wiki ijayo." Mshenga Daudi alitoa taarifa hiyo kwenye kikao kizito ambacho kilimshirikisha Dibwela kama kaka mtu, rafiki zake wawili na wazee wawili kijijini hapo.

Bakari pia, alikuwapo kwenye kikao hicho na yeye alikaa kama mmoja wa wanandugu.

"Labda ni udhuru gani ambao alikuwa nao zaidi kuliko jambo hili kubwa?" Akauliza mzee mmoja.

"Yeye ni mfanyabiashara amesafiri kwenda Mwanza kuchukua bidhaa ambazo ilikuwa ni lazima aende vinginevyo zingetaifishwa na serikali na angepata hasara." Akajibu Billy ambaye siku zote huwa wanafuatana.

Daudi alitoa bahasha na kumkabidhi Dibwela. Bahasha hiyo ilihifadhiwa pesa ya mahari. Kilichotakiwa awali ni laki saba, lakini baada ya kuhesabiwa zilikuwa ni shilingi milioni mbili.

Licha ya pesa zote hizo, lakini Siwatu alionekana mnyonge. Ni kama alikuwa haelewi afanye nini, ingawa hakutoa tamko lolote la kukataa mahari au kukubali.

Mahari ilichukuliwa, Billy na mwenzake Daudi wakaaga kwa furaha, huku wakimwahidi Siwatu kuwa wiki ijayo atamuona mchumba wake.

"Lakini mbona leo kama hana furaha?" Mshenga Daudi alilibaini hilo.

"Anaumwa huyo leo?" Kama mtu Dibwela alidakika haraka haraka ili dada yake asije akajibu jibu ambalo linaweza kuzua balaa.

Kwa bahati nzuri Siwatu hakujibu kitu chochote.

"Bakari umeona?" Siwatu alimlaumu "Yote haya umeyasababisha wewe."

"Sikiliza Siwatu, hapa lawama hakuna. Nimekwambia muda ndiyo utaongea, kama haikuwa riziki yangu basi." Ni jibu ambalo lilimkera Siwatu.

"Mimi hayo majibu yako yananikera hayo?"

"Sasa mimi nifanye nini Siwatu wakati watu wamekuja mpaka hapa wametoa mahari?"

"Tafuta muafaka, wewe mwanaume."

"Muafaka gani tutoroke usiku?"

"Ndiyo, mimi niko tayari kutoroka, nilikuwa tayari kuolewa, lakini kwa sababu umerudi na umesema kile ambacho hata mimi nilikuwa nacho rohoni, siwezi tena kuvumilia. Siwezi kuishi bila wewe. Na hapa ukinyanyua mguu na mimi naondoka. Tunaondoka wote."

"Hutaki tena ndoa?"

"Naitaka, lakini na wewe."

"Watu wameshatoa pesa zao lakini."

Mbona wewe Bakari huelewekі? Si umeniambia kuwa unanipenda na unataka kunioa wakati ulikuwa unajua kabisa kuwa nimechumbiwa. Basi bora usingesema ili mimi niendelee na taratibu za harusi, ukasema 'nawasilisha ombi langu la kutaka kukuoa.' Sasa vipi, au ulikuwa unanijaribu?" Akauliza kwa hasira.

"Hapana mpenzi." Bakari akasogea na kumshika Siwatu. Kwa mara ya kwanza akamshika kama mpenzi wake halisi.

Siwatu alishusha hasira. Akafarijika. Kwa mara ya kwanza akahisi kitu ambacho hakuwahi kukihisi maishani kwake.

Kuitwa mpenzi kwa mara ya kwanza na Bakari kulimfanya kujisikia faraja. Akaangua kilio cha faraja kilichochanganyikana na huzuni.

Anampenda Bakari, lakini papo hapo hakujua afanye nini ili kuepuka kufunga ndoa na mwanaume mwingine ambaye hajawahi kumuona, lakini ni yeye mwenyewe ndiye alikubali kutokana na upweke.

ITAENDELEA JUMAMOSI

HABARI MICHEZO

# AZAM KUIVAA GEITA KWA TAHADHARI

**Na Hadija Mngwai**

AZAM FC imesema kuwa itaivaa Geita Gold Jumapili kwa tahadhari kubwa kwa kuwa wanawajua wapinzani wao hao watakuwa moto katika mchezo huo kutokana na kujeruhiwa mchezo uliopita.


Azam ambayo iliibuka na ushindi wa mabao 2-1 dhidi ya Kagera Sugar itavaana na Geita Gold iliyopoteza dhidi ya Simba katika Uwanja wa Benjamin Mkapa, watakutana kwenye Uwanja wa Azam ulioko Chamazi

Akizungumza na Nipashe, Msemaji wa Azam FC, Thabit Zakaria, amesema kuwa, mechi yao dhidi ya Geita itakuwa ngumu kwa kuwa wapinzani wao hao wametoka kufungwa dhidi ya Simba hivyo wanahitaji kukutana nao kwa tahadhari sana.

"Kikosi chetu kipo vizuri tayari kwa kujiandaa na mchezo wetu dhidi ya Geita Gold siku ya Jumapili lakini tunaenda katika mchezo huo kwa tahadhari kutokana na kuwajua vyema wapinzani wetu," alisema.

"Kwanza ni timu nzuri ambayo ipo katika mashindano ya kimataifa hivyo ina kikosi kizuri cha kiushindani hivyo tutakutana nao kwa tahadhari kubwa ili tuweze kushinda.

"Pia wametoka kufungwa mchezo wao uliopita dhidi ya Simba hivyo watakuja kwa nguvu sana katika mechi hii kutokana na kupoteza, hivyo kocha kwa kuzingatia hayo amekipanga vyema kikosi chake kuelekea mchezo huo."




Mshindi wa Multibet, Gaston Shadrack Mgege kutoka Buza, Dar es Salaam akishikilia mfano wa hundi ya Sh. 24,917,341 baada ya kubashiri kwa usahihi mechi za Multibet kutoka SportPesa. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Manzoki awatuliza Simba

**Na Adam Fungamwango**

STRAIKA wa Vipers ya Uganda 'anayeliliwa' na wanachama na mashabiki wa Simba asajiliwe kwenye timu yao, jana aliwatuliza kwa maneno matamu yaliyoonyesha kuwa yupo pamoja na klabu hiyo na hana mpango wa kwenda popote.

Juzi, mashabiki wa klabu hiyo walichefukwa na kucharuka kwenye mitandao ya kijamii ya michezo hasa baada ya taarifa kuzagaa kuwa huenda angetangazwa jana na watani zao wa jadi Yanga.

"Ni simu maalum kwa mwanangu Nathaniel, natumai utakuja kuwa mfalme wa Simba kama baba yako." Aliposti mchezaji huyo juzi usiku kwenye mtandao wake wa Instagram, wakati wanachama na mashabiki wa Simba wakiwalaumu viongozi wao kwa kuonekana kama vile wanazembea kukamilisha dili hilo.

Kabla mchezaji hiyo kuposti maneno hayo, huku akiweka picha ya Simba mnyama akiwa na mtoto wake kwenye mtandao wake huyo, mmoja wa wajumbe ya Bodi ya Wakurugenzi wa Simba, Crescentius Magori aliweka picha ya mchezaji huyo kwenye mtandao wake wa Instagram na kuandika "Eti Manzoki nini? Wacha hiyo."

Ofisa Mtendaji Mkuu wa klabu hiyo, aliichukua picha ya Manzoki iliyokuwa kwenye akaunti yake ya Instagram naye akaiweka kwake na kuandika maneno haya.

"Usiku mwema Wanasimba. Waliosoma Cuba maelezo mafupi tafadhali."

Kwa kiasi kikubwa posti ya viongozi hao wawili na Manzoki mwenyewe ziliwatuliza wanachama na mashabiki wa Simba ambao walionekana kuchukizwa, kiasi cha baadhi yao kwenda mbali wakidai kama mchezaji huyo akienda Yanga, basi viongozi wajiuzulu.

Taarifa za Manzoki kujiunga na Yanga zilianza kuzagaa kwenye mitandao mbalimbali ya kijamii na ikapata nguvu zilipochapostiwa picha za Makamu Mwenyekiti wa klabu hiyo, Arafat Haji alionekana yupo nchini Uganda na Kocha Mkuu wa timu ya taifa ya nchi hiyo aliyewahi pia kuwa kocha wa Yanga, Mserbia Milutin Sredojevic 'Micho'.

Kuwepo kwa mkutano kati ya Yanga na Waandishi wa Habari nako kuliwavuruga mno Wanasimba wakidhani kuwa ni wa kumtambulisha mchezaji huyo.

Mchezaji huyo ambaye kwa sasa ana mgogoro wa kimkataba na klabu yake, amekuwa hachezi mechi yoyote kupinga maelezo yao kuwa ana mkataba wa miaka miwili, huku mwenyewe akidai ni miezi miwili.

Tetesi zinadai kuwa Manzoki amekataa kuuzwa kwenye klabu yoyote ile zaidi ya Simba, ambayo anaisuburia kama dili linaweza kumalizika msimu huu au dirisha dogo la usajili.

## Polisi FC Zanzibar yapata udhamini

**Na Faustine Shija**

KAMPUNI ya GF Truck ya Dar es Salaam imeingia mkataba wa udhamini kwa klabu ya Polisi Zanzibar inayoshiriki Ligi Kuu visiwani humo.

Akizungumza wakati wa hafla ya kuikabidhi vifaa mbalimbali vya michezo kwa timu hiyo Ofisa Masoko Mkuu wa Kampuni ya GF Trucks & Equipments Ltd, Salman Karmal alisema Zanzibar kuna vipaji vingi lakini kutokana na ligi hiyo kukosa wadhamini vipaji vingi vinapotea lakini ujio wa kampuni kama ya Azam, Benki ya Watu wa Zanzibar (PBZ) kumeamsha hali na morali wa ligi hiyo kufatiliwa na watu tofauti.

Alisema kwa kuona hilo, kampuni hiyo imeamua kujitosa kwenye ligi hiyo na kwa kuanzia wameanza kuidhamini klabu hiyo ya Jeshi la Polisi Zanzibar.

"Mkataba huu wa mwaka mmoja utaipa fursa klabu ya Polisi kupata vifaa vyote vinavyoitajika kwenye timu, lengo ni kuisaidia kufanya vizuri kwenye ligi huku ikiwa kwenye mazingira mazuri," alisema Karmal.

Alisema udhamini huo pia ni sehemu moja wapo ya kuunga mkono juhudi za Rais wa Zanzibar Hussein Mwinyi katika kuhakikisha sera ya michezo inatimizwa kwa vitendo.

"Tulianza udhamini katika soka kwa kuidhamini Mbao FC ya Mwanza ambayo ilishuka daraja, faida yake tuliiona na msimu huu tumeidhamini Singida Big Stars, tumeona ni vyema pia kuja Zanzibar kuunga mkono juhudi za kulitangaza soka la Zanzibar na kuunga juhudi za serikali kuhakikisha sera ya michezo inatekeleza kwa vitendo," alisema Karmal.

Kwa upande wake Mwenyekiti wa klabu ya Polisi CP Hamad Khamis Hamad aliishukuru kampuni ya GF kwa Kuidhamini timu hiyo huku akiahidi kunitumia vyema udhamini huo.

Aidha, alisema udhamini huo utalipunguzia mzigo Jeshi la Polisi katika kuhudumia timu hiyo.

"Udhamini huu utaongeza morali kwa wachezaji pia, na kwa kuthamini hiki walichokifanya GF Truck tutahakikisha tunafanya vizuri kwenye ligi," alisema CP Hamad.

Pia alizitaka kampuni nyingine kuiga mfano wa GF Truck kwa kuthamini vilabu vya taasisi za serikali ili kuviwezesha kufanya vizuri.

## Singida kuendeleza dozi kwa Mbeya City

**Na Hadija Mngwai**

SINGIDA Big Star chini ya kocha wake Hans Pluijm imetamba kuendeleza dozi katika uwanja wake wa nyumbani kwa kuifunga Mbeya City siku ya Jumapili.

Singida ambayo ilifanikiwa kuanza vyema mchezo wake wa awali wa Ligi Kuu Bara kwa kuifunga Tanzania Prisons bao 1-0, itaikaribisha Mbeya City katika uwanja wake wa nyumbani Jumapili ikiwa ni mchezo wa mzunguko wa pili.

Akizungumza na Nipashe, Ofisa Habari wa Singida United, Hussein Massanza amesema kuwa, kikosi chao kipo vizuri kwa ajili ya mchezo wa Jumapili licha ya kuwa na majeruhi mmoja Abdul Mangalu lakini wana imani ya kushinda uwanja wa nyumbani.

"Kikosi kipo vizuri kuelekea mchezo wetu wa Jumapili mwalimu anaendelea kukiweka sawa kikosi na moja ya mikakati ni kuhakikisha tunashinda katika uwanja wa nyumbani.

" Tuna majeruhi mmoja beki wetu Abdul Mangalo ameumia kifundo cha mguu katika mchezo wetu uliopita dhidi ya Tanzania Prisons na anaendelea na matibabu chini ya madaktari wetu.

"Kikosi kwa ujumla kipo fiti kuelekea mchezo wetu wa Jumapili na tunaimani tutashinda," alisema Massanza.

## ZISIKUPITE

### AUBAMEYANG KUBAKI

PIERRE-Emerick Aubameyang anataka kupigania nafasi yake katika klabu ya Barcelona, ambayo imekataa dau la pauni milioni 12 kutoka kwa Chelsea kumnunua mshambuliaji huyo wa Gabon mwenye umri wa miaka 33. ***(Deportivo Mundo via Mirror)***

### MESSI ATAKIWA BARCA

KOCHA wa Barcelona, Xavi ameiomba Barcelona kumsajili tena mshambuliaji wa Argentina, Lionel Messi mwenye umri wa miaka 35, kutoka Paris St-Germain. ***(Sun)***

### CAICEDO AGOMBEWA

KLABU ya Manchester United imejiunga na orodha ya Klabu za Ligi Kuu England ikiwamo Arsenal na West Ham, zinazotaka kumsajili kiungo wa kati wa Ecuador, Moises Caicedo mwenye umri wa miaka 20 kutoka Brighton. ***(Mirror)***

### TIELEMANS ARUHUSIWA

KLABU ya Leicester City ipo tayari kuruhusu Arsenal kumsaka kiungo wa kati wa Ubelgiji, Youri Tielemans mwenye umri wa miaka 25 kuondoka bila malipo msimu ujao. ***(Times)***

### GUIRASSY AWANIWA

KLABU ya Everton imetoa ofa kwa mshambuliaji wa Rennes na Guinea, Serhou Guirassy mwenye umri wa miaka 26. ***(Mail)***

### BERG ATAKIWA

KLABU ya Blackburn inaongoza harakati za kumsajili beki wa kati wa Uholanzi, Sepp van den Berg mwenye umri wa miaka 20 kwa mkopo kutoka Liverpool. ***(Sun)***

### EMERSON AULIZIWA

KLABU ya Nice imeulizia kuhusu beki wa kushoto wa Chelsea na Brazil, Emerson Palmieri mwenye umri wa miaka 28. ***(Fabrice Hawkins via Get French Football News)***

### SILVA HAUZWI

KLABU ya Manchester City haitaki kumuuza kiungo wao Bernardo Silva mwenye umri wa miaka 28, licha ya Paris St-Germain na Barcelona kumtaka mchezaji huyo wa kimataifa wa Ureno. (Sky Sports)

### GAKPO HAUZWI

KLABU ya PSV Eindhoven haitakaribisha ofa kutoka kwa Manchester United kumnunua mshambuliaji wa Uholanzi, Cody Gakpo mwenye umri wa miaka 23. ***(MailOnline)***

### CARRASCO AFIKIRIWA

KLABU ya Manchester United inafikiria kumnunua mshambuliaji wa Atletico Madrid na Ubelgiji, Yannick Carrasco mwenye umri wa miaka 28 kwa pauni milioni 25. ***(Telegraph)***

### WINKS HATAKIWI

KLABU ya Everton ilikuwa ikihusishwa na kiungo wa Tottenham Hotspur, Harry Winks mwenye umri wa miaka 26, lakini kocha Frank Lampard ameamua kuachana na mpango huo. ***(Times)***

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# CASEMIRO HUYO MAN UTD

**MANCHESTER,** England

## Kulipwa mshahara mkubwa, kusaini miaka mitano na...

KLABU ya Manchester United imekubaliana kimsingi na Casemiro na wanakaribia kumsajili kiungo huyo wa kati wa Brazil kutoka Real Madrid, kwa mujibu wa 90min.

United wamehamia kwa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 30 ambaye ni mshindi wa mara nyingi wa Ligi ya Mabingwa Ulaya wiki hii na wanatazamiwa kulipa euro milioni 60, pamoja na nyongeza ya euro milioni 10 ili kukamilisha dili hilo.

Uhamisho huo unatarajiwa kukamilika wiki ijayo na anatarajiwa kufanyiwa vipimo vya afya ndani ya saa 24 zijazo.

90min iliripoti Alhamisi kwamba mchezaji huyo alipewa mkataba wa miaka mitano na chaguo la kuongezwa kwa miezi 12.

Anatarajiwa kulipwa kiasi cha pauni 400,000 kwa wiki, pamoja na bonasi.

Kwa mujibu wa 90min Casemiro alikuwa anaona hana nafasi kule Madrid kufuatia kusajiliwa kwa Aurelien Tchouameni na Eduardo Camavinga.

Real walikuwa wamepanga na mchezaji huyo kwa msimu mpya, lakini Casemiro amekuwa na hamu ya kucheza England kwa muda na amechangamkia fursa hiyo.

Heshima ya Real kwa Casemiro na matakwa yake imefanya mpango huo kuwa rahisi kuendeleza, na hawakutaka kusimama katika njia yake.

Casemiro angehitaji kusajiliwa ifikapo saa 12 jioni jana ya Ijumaa ili kucheza mechi ijayo ya United ya Ligi Kuu England dhidi ya Liverpool.


BREAKING NEWS
SUPA JACKPOT KWA 1000/- 1,023

MECHI KALI
COASTAL UNION
VERSUS
YOUNG AFRICANS
1 | 7.06
X | 3.48
2 | 1.49

KUWEKA PESA:
- PIGA *150*87#, CHAGUA 4
- WEKA PESA.
tigo pesa
vodacom m-pesa
BREAKING
airtel money
ZANTEL EZYPESA
SEND

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#
GBT:0249 18+ HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA: 0764115588, 0677115588 0685115588
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# NEVILLE AMSIHI RONALDO



**MANCHESTER,** England

BEKI wa zamani wa Manchester United, Gary Neville, amemsihi fowadi wa Man United Cristiano Ronaldo, kusimama na kuzungumza matatizo ya timu hiyo.

Ronaldo, 37, ameweka wazi anataka kuzungumza na waandishi wa habari kwa kina ili kufichua mambo yanaoendelea ndani ya klabu hiyo.

Ronaldo aliandika kwamba baada ya wiki mbili atazungumza kuweka ukweli wote kuhusu hatima yake Old Trafford.

Aidha, Neville alimjibu kupitia ukurusa wake wa Twitter "Kwanini mchezaji bora zaidi wa wakati wote (kwa maoni yangu) analazimika kusubiri wiki mbili ili kuwaambia mashabiki wa Manchester United ukweli? "Simama sasa uzungumze, klabu iko kwenye mgogoro na inahitaji viongozi wa kuongoza".

Nyota Ronaldo, mshindi mara tano wa tuzo ya Ballon d'Or anataka kuondoka Old Trafford kutokana na ukweli kwamba anataka kujiunga na timu inayoshiriki Ligi Mabingwa Ulaya msimu.

# Delle Alli huyo Besiktas



**LIVEPOOL,** England

KIUNGO wa Everton Dele Alli mwenye umri wa miaka 26, yupo mbioni kukamilisha uhamisho wake wa kujiunga na Besiktas, kwa mkopo ndani ya saa chache, kwa mujibu wa ripoti.

Nyota huyo alikuwa na matumaini ya kukiwasha Everton chini ya Frank Lampard akitokea Tottenham lakini kiwango chake hakijaridhisha.

Dele Alli ameonyesha nia ya kuondoka Everton baada ya ujio wa kiungo Amadou Onana aliyesajiliwa na Lampard.

Kwa mujibu wa ripoti, Besiktas inataka kumsajili kwa mkopo wa msimu mzima sasa uhamisho huo unaelekea kukamilika baada ya Dele Alli kukubali.

Dele Alli alikuwa mchezaji wa kiwango cha juu wakati alipokuwa akikipiga Tottenham kabla ya kiwango chake kushuka. Ikumbukwe nyota huyo wa Kimataifa England aliwahi kubeba tuzo ya PFA mara mbili kipindi alipokuwa moto wa kuotea mbali.

## HABARI MICHEZO

,154,178

SUPA JACKPOT
MECHI WIKI HII
BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 20/08/22 | 17:00 | Crystal Palace vs Aston Villa | 2.53 | 3.23 | 2.78 |
| 02. 20/08/22 | 17:00 | Fulham vs Brentford | 2.39 | 3.28 | 2.93 |
| 03. 20/08/22 | 17:00 | Preston vs Watford | 2.89 | 3.14 | 2.49 |
| 04. 20/08/22 | 17:00 | Birmingham vs Wigan | 2.41 | 3.18 | 2.98 |
| 05. 20/08/22 | 17:00 | Swansea vs Luton Town | 2.41 | 3.18 | 2.98 |
| 06. 20/08/22 | 17:00 | Bolton vs Sheffield Wed | 2.85 | 3.39 | 2.39 |
| 07. 20/08/22 | 17:00 | Forest Green vs Plymouth | 2.70 | 3.40 | 2.50 |
| 08. 20/08/22 | 17:00 | Burton vs Port Vale | 2.31 | 3.38 | 2.98 |
| 09. 20/08/22 | 17:00 | Doncaster vs Salford City | 2.63 | 3.28 | 2.63 |
| 10. 20/08/22 | 17:00 | Colchester vs Leyton Orient | 2.98 | 3.33 | 2.33 |
| 11. 20/08/22 | 17:00 | Crawley Town vs AFC Wimbledon | 2.43 | 3.24 | 2.89 |
| 12. 20/08/22 | 17:00 | Mansfield vs Stockport | 2.25 | 3.49 | 2.99 |
| 13. 20/08/22 | 17:00 | Dundee Utd vs St. Mirren | 2.31 | 3.09 | 3.24 |
| 14. 20/08/22 | 17:00 | Motherwell vs Livingston | 2.25 | 3.13 | 3.33 |
| 15. 20/08/22 | 17:00 | Ross County vs Kilmarnock | 2.26 | 3.14 | 3.29 |
| 16. 20/08/22 | 17:00 | St. Johnstone vs Aberdeen | 2.93 | 2.98 | 2.58 |
| 17. 20/08/22 | 17:00 | Hamilton vs Raith Rovers | 2.43 | 3.14 | 2.99 |

MECHI ZA USHINDI
"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE "2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

JUMAMOSI - 20 - AGOSTI 2022

| MUDA | GAME ID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 12:00 | 1655 | Shimizu S Pulse vs Kashiwa Reysol | 2.44 | 3.14 | 2.69 |
| 14:30 | 1290 | Tottenham vs Wolverhampton | 1.37 | 4.69 | 7.38 |
| 14:30 | 2849 | Shanghai SIPG vs Hangzhou NG | 1.90 | 3.49 | 3.49 |
| 14:30 | 4273 | Hibernian vs Rangers | 5.41 | 3.86 | 1.58 |
| 15:00 | 3976 | FK Khimki vs Lokomotiv Moscow | 2.70 | 3.30 | 2.46 |
| 16:00 | 2079 | Coastal Union vs Young Africans | 7.06 | 3.48 | 1.49 |
| 16:00 | 2472 | Golden Arrows vs TS Galaxy FC | 1.92 | 3.05 | 4.31 |
| 16:00 | 3120 | FS Metta/Lu vs Spartaks Jurmala | 2.57 | 3.26 | 2.47 |
| 16:00 | 4009 | Sekhukhune United vs Mamelodi Sundowns | 4.99 | 3.29 | 1.74 |
| 16:30 | 1675 | VfL Wolfsburg vs Schalke 04 | 1.80 | 3.75 | 3.89 |
| 16:30 | 2746 | Bayer Leverkusen vs Hoffenheim | 1.65 | 4.21 | 4.21 |
| 16:30 | 3528 | Augsburg vs Mainz | 3.31 | 3.36 | 2.08 |
| 16:30 | 4818 | Borussia Dortmund vs Werder Bremen | 1.37 | 5.19 | 6.39 |
| 16:30 | 5449 | Stuttgart vs SC Freiburg | 2.60 | 3.40 | 2.50 |
| 17:00 | 1665 | St Johnstone vs Aberdeen | 3.37 | 3.01 | 2.24 |
| 17:00 | 1981 | Crystal Palace vs Aston Villa | 2.45 | 3.19 | 2.79 |
| 17:00 | 2886 | QPR vs Rotherham | 2.07 | 3.26 | 3.46 |
| 17:00 | 2936 | Midtjylland vs Aarhus | 1.68 | 3.87 | 4.52 |
| 17:00 | 3402 | Everton vs Nottingham | 1.90 | 3.40 | 3.85 |
| 17:00 | 3711 | Fulham vs Brentford | 2.38 | 3.30 | 2.80 |
| 17:00 | 4296 | Birmingham vs Wigan | 2.42 | 3.15 | 2.85 |
| 17:00 | 4672 | Leicester vs Southampton | 1.80 | 3.76 | 3.86 |
| 17:00 | 4812 | Sheffield Utd vs Blackburn | 1.79 | 3.41 | 4.41 |
| 17:00 | 5199 | Motherwell vs Livingston | 2.30 | 3.07 | 3.17 |
| 17:30 | 5401 | Dinamo Moscow vs Spartak Moscow | 2.55 | 3.30 | 2.60 |
| 18:00 | 1514 | Monaco vs Lens | 1.75 | 3.82 | 4.13 |
| 18:00 | 5224 | RB Salzburg vs Austria Klagenfurt | 1.10 | 7.68 | 15.76 |
| 18:15 | 2419 | Simba vs Kagera Sugar | 1.38 | 4.02 | 7.84 |
| 18:30 | 5187 | Osasuna vs Cadiz CF | 1.93 | 3.23 | 4.14 |
| 18:30 | 5768 | Cape Town City vs Stellenbosch | 2.22 | 2.90 | 3.50 |
| 19:00 | 4089 | Bodo Glimt vs Ham-Kam | 1.22 | 6.45 | 10.07 |
| 19:15 | 1184 | Hatayspor vs Gaziantep BB | 2.06 | 3.47 | 3.32 |
| 19:30 | 1425 | Torino vs Lazio | 2.89 | 3.34 | 2.30 |
| 19:30 | 1941 | Udinese vs Salernitana | 1.72 | 3.76 | 4.32 |
| 19:30 | 4508 | Union Berlin vs RB Leipzig | 3.40 | 3.35 | 2.05 |
| 19:30 | 5873 | Bournemouth vs Arsenal | 6.55 | 4.20 | 1.45 |
| 20:00 | 2364 | Samsunspor vs Eyupspor | 2.45 | 3.33 | 2.55 |
| 20:30 | 3062 | Mallorca vs Betis | 3.03 | 3.13 | 2.38 |
| 20:30 | 5846 | Sturm Graz vs LASK Linz | 2.38 | 3.24 | 2.70 |
| 21:00 | 1647 | Maritzburg Utd vs Chippa Utd | 2.29 | 2.75 | 3.59 |
| 21:15 | 2678 | Luka Koper vs Olimpija Ljubljana | 2.43 | 3.23 | 2.64 |
| 21:30 | 1321 | Lamia vs AEK Athens | 6.63 | 3.72 | 1.53 |
| 21:45 | 2518 | Sassuolo vs Lecce | 1.76 | 3.84 | 3.99 |
| 21:45 | 2990 | Antalyaspor vs Trabzonspor | 2.56 | 3.16 | 2.71 |
| 21:45 | 4189 | Inter vs Spezia | 1.16 | 7.01 | 13.02 |
| 22:00 | 2535 | Marseille vs Nantes | 1.58 | 3.98 | 5.24 |
| 22:00 | 4388 | Emmen vs Utrecht | 3.11 | 3.31 | 2.19 |
| 22:05 | 2617 | Dinamo Zagreb vs NK Osijek | 1.53 | 3.81 | 5.48 |
| 22:30 | 5924 | Porto vs Sporting Lisbon | 2.07 | 3.37 | 3.37 |
| 23:00 | 3002 | Celta Vigo vs Real Madrid | 4.55 | 4.04 | 1.66 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# WAAMUZI 70 KUFANYA MTIHANI WA UTIMAMU LEO

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

JUMLA ya waamuzi 70 wanatarajia kufanya mtihani wa utimamu wa mwili kuelekea msimu mpya wa Ligi Kuu ya Zanzibar inayodhaminiwa na PBZ.

Kati ya waamuzi hao 40 ni kutoka Unguja na 30 kutokea Kanda ya Pemba.

Mtihani huo unatarajia kufanyika Jumapili ambapo leo kutakuwa na zoezi la upimaji afya kwa waamuzi watakaofanya mtihani huo.

Mtihani huo unatarajia kushirikisha waamuzi kutoka mikoa mitatu ya Unguja, wakati kwa waamuzi wa mikoa miwili ya Pemba watafanya baada ya kumalizika zoezi hilo hapa Unguja ambapo itakuwa Agosti 26.

Akizungumza na gazeti hili, Katibu wa Kamati ya Waamuzi wa ZFF, Ali Juma Kombo, alisema mpaka sasa maandalizi yote yamekamilika kuelekea mtihani huo.

Alisema kuwa leo daktari mkuu wa michezo atasimamia zoezi la kupima afya kama ilivyo taratibu za mtihami huo ili kuhakikisha watakaofanya kazi hiyo wapo salama kiafya.

"Kesho (leo) litakuwa zoezi la kupima afya kwa waamuzi wetu ambao watakaofanya mtihani huo, kama tunavyojua kwa mujibu wataratibu lazima tucheki, presha, sukari, uzito pamoja na vipimo vingine," alisema Kombo.

Aidha alisema waamuzi ambao hawatafanya vizuri katika mitihani yote miwili ikiwamo ya uwanjani na sheria za soka hawataruhusiwa kuchezesha Ligi Kuu, Ligi Daraja la Kwanza na Kombe la FA.



Baadhi ya wachezaji wa Timu ya Soka ya Planet Sports Club ya Luguruni Dar es Salaam, wakiwa mazoeni katika uwanja wao juzi. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Yanga yapata dili mpya

**Na Shufaa Lyimo**

KLABU ya Yanga jana imesaini mkataba wa uhusiano wa miaka miwili na kampuni ya kimasoko ya Jackson Group jijini Dar es Salaam jana.

Akizungumza jijini jana Rais wa Klabu hiyo, Hersi Said, alisema amefurahi kusaini mkataba huo ambapo ameweka wazi kuwa umefungua milango ya asilimia 49 za hisa zitakwenda kwa mwekezaji na asilimia 51 kwa wanachama.

"Nimefurahi kuingia makubaliano ya kibiashara na kampuni hii nina amini utaleta mfumo wa kisasa wa biashara ndani ya klabu yetu, alisema Said.

Alisema anaipongeza kampuni hiyo kupata bafasi ya kufanya nao kazi na kuahidi kushirikiana kwenye kila jambo la kimasoko ikiwamo kutumia nguvu nyingi ili waweze kujenga uwanja, kama alivyoahidi kwenye kampeni zake.

Rais huyo alisema kampuni hiyo ina mamlaka ya kuitafutia biashara klabu hiyo jambo ambalo limewafanya waridhike kusaini mkataba huo.

"Huu mkataba ni wa mahusiano ninaomba kila mtu aelewe si wa pesa bali kampuni ya Jackson Group ndio ambao wanatutafutia sisi pesa," alisema rais huyo.

Alisema mkutano mkuu ulipitisha mfumo wa mabadiliko hivyo hatujapenda kuajiri mtu ambaye atalipwa kutokana na idara hiyo na kuamua kutafuta kampuni, ambayo anafahamu faida zake.

Alisema Yanga ni taasisi kubwa ambayo inapaswa kuendeshwa kisasa kwani amesema klabu hiyo ni kongwe isipokuwa maendeleo yaliyopo hayaendani na ukubwa wake.

Vile vile alisema mpaka sasa wamepokea barua za maombi 700 ambazo zimepelekwa na watu mbali mbali wakiomba uongozi ndani ya timu hiyo.

Naye Mkurugenzi wa kampuni hiyo, Kelvin Twisa alisema ameamua kuingia makubaliano hayo kutokana na kuwa Yanga ni timu ambayo imebeba mataji mengi msimu uliopita na kudai wapo tayari kufanya biashara na taasisi nyingine hapa nchini.

"Nimefurahi kufanya kazi na Yanga ni klabu ambayo imepata mataji mengi msimu uliopita ninaamini tutapata mafanikio pande zote mbili," alisema Twisa.




Casemiro huyo Man United

UKURASA 21


Wachezaji wa Simba wakiwa mazoezini.

# Mnigeria kutua Simba

## ●●● Anakuja kuchukua nafasi ya Akpan ambaye kocha hajaridhishwa naye na...

**Na Saada Akida**

WAKATI Simba ikiwa na kibarua cha kusaka pointi tatu dhidi ya Kagera Sugar, mchezo wa pili wa Ligi Kuu Tanzania Bara, tayari viongozi wa wekundu wa Msimbazi wapo katika mchakato wa kumalizana na kiungo mkabaji wa Rivers United ya Nigeria, Morice Chukwu.

**Nyota huyo yupo katika ma zungumzo na uongozi wa Simba kwa ajili ya kukamilisha dili lake na kutua nchini kwa ajili ya kuchukua nafasi ya Victor Akpan.**

Akpan, alisajiliwa msimu huu ndani ya Simba na kupelekwa kwa mkopo Coastal Union baada ya Kocha Mkuu wa Wekundu wa Msimbazi hao, Zoran Manojkovic kumwondoa kikosini nyota huyo na kuhitaji kiungo mkabaji ambaye anatajwa kuwa ni Chukwu.

Kwa mujibu wa chanzo chetu mazungumzo baina ya Simba na Chukwu yanaenda vizuri na muda wowote watamtambulisha nyota huyo.

"Ni kweli Akpan anapelekwa kwa mkopo na nafasi yake itachukuliwa na Chukwu ambayo yuko katika hatua ya mwisho ya makubaliano na muda wowote atasaini mkataba na kutumikia Simba," alisema mtoa habari huyo.

Meneja wa Idara ya Habari na Mawasiliano wa Simba, Ahmed Ally alisema zoezi la usajili litafanyika kulingana na mapendekezo ya Kocha Maki kuhitaji kiungo mkabaji na mshambuliaji.

Alisema dirisha la usajili bado liko wazi, Maki amepewa uhuru wa kuangalia kama anahitaji maboresho na mlango uko wazi wa kuangalia mchezaji gani anamuhitaji kwa ajili ya kuboresha timu yake.

"Tulishamaliza usajili, lakini viongozi walitoa nafasi kwa Kocha Maki kuangalia kikosi chake, alipata muda wa kuiona timu yake na kuona anahitaji kiungo mkabaji na mshambuliaji, hali hiyo ndiyo linaweza kutokea kwa sababu ya dirisha la usajili bado liko wazi," alisema Ahmed.

"Kuhusu mshambuliaji wa Vipers, Cesar Manzoki, tusubiri muda utaongea, masuala ya kawaida katika usajili ni mapema hasa mchezaji anapotajwa na Simba wengine kudakia lakini tutaona mwisho wake," alisema Ahmed Ally.

Huku usajili ukiendelea kwa Simba kufanyia kazi mahitaji ya kocha wao Maki, kikosi cha timu hiyo kitakuwa na kibarua kigumu dhidi ya Kagera Sugar.

Makocha wa timu ya Simba, Seleman Matola na Kagera Sugar, Francis Baraza kuelekea mchezo wa leo wa Ligi Kuu Tanzania Bara utakaopigwa katika Uwanja wa Benjamin Mkapa saa 12:15 jioni, wote walitamba kuibuka na ushindi.

Matola alisema, wamejipanga kupata matokeo mazuri dhidi ya wapinzani wao ambao wamekuwa wakiwasumbua kwa kwa misimu miwili iliyopita.

Alisema, hakuna mchezaji majeruhi na sasa kazi iliyobaki ni vijana wao kwenda kupambana kwa ajili ya kutafuta pointi tatu muhimu katika mchezo huo.

"Tumefanyia kazi mapungufu ya mechi iliyopita na kuhusu safu ya ushambuliaji iko vizuri na wachezaji wako tayari kwa ajili ya kupambana kutafuta pointi tatu katika mchezo wa kesho (leo)," alisema Matola.

Nahodha wa Simba, Shomari Kapombe, alisema wamejiandaa vizuri makocha wameshamaliza kazi yao kilichobakia wao kwenda kuwapa furaha mashabiki kwa kushinda mchezo huo.

"Tumejiandaa vizuri, mechi haitakuwa rahisi kwa sababu tunapokutana na Kagera Sugar mchezo unakuwa wa ushindani mkubwa na tumejipanga kuendelea kutafuta pointi tatu katika mchezo wa kesho (leo)," alisema Kapombe.

Naye Kocha Baraza alisema wamejiandaa vizuri na wanawaheshimu Simba kwa sababu bado ni timu bora.

Alisema, kulingana ubora wa wapinzani wake anatarajia kutumia viungo kwa ajili ya kuendelea kuisumbua Simba kama ilivyo kwa msimu miwili iliyopita.

"Bado timu yangu haijakaa sawa kwa sababu ya wachezaji wengi wapya lakini hatutakuwa rahisi kwa Simba, tutaenda kupambana kwa ajili ya kutafuta matokeo mazuri katika mchezo wetu wa pili," alisema Baraza.

# Yanga kibaruani kwa Coastal leo

**Na Adam Fungamwango**

MABINGWA watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara, leo watajitupa tena kwenye Uwanja wa Sheikh Amri Abeid, jijini Arusha kuzisaka pointi tatu dhidi ya timu korofi ya Coastal Union.

Mara ya mwisho timu hizo zilikutana kwenye uwanja huo huo Julai 2, mwaka huu, iilipocheza fainali ya Kombe la FA timu hizo zikatoka sare ya mabao 3-3 kwenye mechi ya kusisimua ambapo mshindi alilazimika kupatikana kwa mikwaju ya penalti, Yanga ikishinda kwa matuta 4-1.

Pia timu hizo zilicheza mechi za kwanza kwenye uwanja huo huo, Yanga ikikipiga Jumanne iliyopita dhidi ya Polisi Tanzania na kushinda mabao 2-1, Coastal ikicheza kesho yake Jumatano dhidi ya KMC na kushinda kwa bao 1-0.

Kocha Mkuu wa Yanga, Mtunisia Nasreddine Nabi, alikiri mechi itakuwa ngumu kwa sababu huwa hivyo kila wanapokutana nayo.

"Baada ya kucheza dhidi ya Polisi Tanzania tulibaki hapa ili kupata muda wa kupumzika na tuna imani kuwa tumejiandaa vyema kwa ajili ya mechi hii. Kuelekea kwenye mchezo huo tunajua mechi zote tulizocheza dhidi ya Coastal Union huwa ni ngumu na pia tumewaona wakicheza dhidi ya KMC, tunaamini ni msimu huu ni wazuri zaidi kuliko hata msimu uliopita," alisema Nabi.

Hata hivyo alisema wanakwenda kucheza mechi hiyo wakiwakosa wachezaji watatu, Lazrous Kambole, kipa Djigui Diarra na kiungo Salum Aboubakar 'Sure Boy' ambaye aliumia kwenye mechi ya Ngao ya Jamii dhidi ya Simba.

"Tuna wachezaji wapya naona wameshaanza kuzoea hali ya hewa, mpira wa Tanzania na kuzoeana na wenzao wanatakiwa kupewa muda nadhani baada ya michezo mitatu ndiyo tuanze kuwajadili," alisema kocha huyo.

Naye Kocha Mkuu wa Coastal Union, Juma Mgunda, alisema walivyojiandaa kucheza na KMC, sivyo walivyojiandaa kucheza dhidi ya Yanga.

"Kwa ufupi maandalizi yamekamilika, tunakwenda kucheza na Yanga ni timu nzuri, imesajili vizuri na inajiandaa kuiwakilisha nchi kwenye michuano ya kimataifa kwa hiyo ni lazima tuwe na maandalizi mazuri, jinsi gani ya kukabilina na timu kama hiyo maandalizi yake yamekamilika. Kwa bahati nzuri wachezaji wangu wote wako fiti, hakuna majeruhi," alisema Mgunda.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >